

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**(CKRC)**

**VERBATIM REPORT OF**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,**

**SHINYALU CONSTITUENCY,**

**ST. PHILLIPS CHURCH HALL, MUKOMARI**

**ON**

**1<sup>st</sup> August 2002**

**PROCEEDINGS OF CONSTITUENCY HEARINGS, SHINYALU CONSTITUENCY, HELD AT ST. PHILLIPS  
CHURCH HALL, MUKOMARI ON 01.08.02**

**PRESENT:**

Mr. Charles Maranga - Commissioner

**SECRETARIAT STAFF IN ATTENDANCE:**

Fatuma Issa - Programme Officer  
Wambeyi Makomere - Assistant Programme Officer  
Mary Babu - Verbatim Recorder  
Mr. Majanja - District Coordinator  
  
Martin Musonye - Chairman CCC  
Tom Shiyachi - Member CCC

The meeting was called to order at 10.10 a.m. by Commissioner Maranga as the Chair.

**Martin Musonye:** Wageni wetu wamefika leo, Bwana Commissioner wa CKRC na wengine wote ambao wako hapa, hamujamboni? Nachukua nafasi hii kumukaribisha nyinyi nyote hapa St. Philips Catholic Church na kabla hatujaendelea sana ningependa tuanze na maombi ambaye inatolewa na mmoja wetu Bwana Tom Shivachi.

**Tom Shivachi:** Baba, ni asante Mungu wetu Mungu wa rehema na upendo nakushukuru kwa sababu umetuwezesha kuamuka ashubuhi kuja kukutana hapa, mfalme wa mfalme wewe uliumba dunia ukaumba na watu ukawapa nafasi ya kujitawala na kwa hivyo Baba tunapokuja mbele zako tunakuomba utupatie marifa yale ambaye tunasema Bwana yawe matakatifu mbele zako na yote atakayo andikwo Baba yawe na ushindi wa kulete amani katikati ya watu wako. Naomba haya katika jina ya Yesu Kristu aliye mukombozi wetu. Amen.

**Martin Musonye:** Asante. Vile kupoteza wakati mwingi nafikiri nyinyi nyote munajua ni nini haswa imemuleta hapa na ningependa labda wakati huu nimujulisha kwa wageni wetu ambao nitauliza wajitambulisha kwa majina na kazi zao halafu upande wa administration na offisi ya CCC na tuendele.

**Com. Maranga:** I think it will be the other way round, mimi ningetaka wewe kwa ufupi kabisa kujitambulisha na watu wako halafu uite vile vile Bwana DO ahutubie wananchi wa sehemu hii halafu urudisha mika pande hii halafu nitajitambulisha hawa wengine.

**Martin Musonye:** Sasa, kwa kamati yetu ya Shinyalu constituency Constitutional Committee, sisi huwa watu tisa kwa jumla na wale wako hapa kwa sasa tuko watatu. Mimi ningependa kutambua Bi Zipporah Musonye kama mwana kamati, Bwana Tom Shivachi kama mwana kamati na mimi mwenyewe naitwa Martin Musonye nido mwenyekiti. Sasa wakati huu ningepeda mukaribishe Bwana DO.

**DO:** Thank you very much Mr. Musonye, Honorable Commissioner from the Constitutional Review Commission of Kenya, Commission representative officials, Chiefs ambao wako hapa, wananchi wa eneo hili la Shinyalu. Hamujambo? (kiluyah)

Bwana Commissioner ama Honorable Commissioner, na tuko hapa saa hii kumukaribisha wewe .....yako upande wa Shinyalu na tuko tayari hapa, wananchi wako tayari kupeana their own views regarding the Constitutional Review. Upande huu ni watu wamekuja, ni wachache but pengine wametumwa wamekuja na memorandum so inaweza inakua ni mtu moja anawakilisha pengine watu hamsini na tulifanya publicity na Bwana Musonye vizuri sana na I am sure you will get the views. Ile kitu ningependa kuwaomba wananchi wa hapa you should be very brief na sijui kama, not even brief, to the point. Mwendako akiwa ametoa maoni yake hapana rudia sawa sawa? Hapa rudia.

Lakini hatukatazi nyinyi, ukiwa na uwezo ama nafasi sawa sawa lakini hapana rudia na tutoe maoni yetu kwa njia ambayo ni ya utulivu tusivutane na mwenzako akepeana maoni musianze kupigia makofi amakushambulia sana hiyo ndio njia moja ya kupoteza wakati na si muzuri. Hatukatazi nyinyi mupige makofi lakini ni nzuri lakini kuiga ni moja tu. Sijui nafikiria Bwana Commissioner in other areas wanapiga makofi ama mtu anashangiliwa sana? Commissioner, we are very late, tuko tayari kuendelea wananchi wa hapa kwa kawaida ni watulivu and they are very late now. Waliniambia wanagojea wewe kwa ili uingia hapa na kupokea maoni yao so that you can take to the higher authorities. Lakini mujue hii ni Katiba si ndio, hii ni Marekebisha ya Katiba so munapotoa maoni hapa mutoe maoni ya kusaidia nyinyi siku ijazo, siasa, jami na kiuchumi. Mumelewa hivo? So, unatengeneza maisha yako ya siku ijazo na watoto na kila mtu ambao watakuweko nchi hii siku ijazo.

Na ni mzuri kutengeneza Katiba ambayo inaweza kudumu miaka mingi bila kurekebisha tena, ni nzuri kurekebisha kulingana na social changes or political or economic changes lakini ukiona kama ya America nafikiria imerekebisha pengine over 200 years old, 1786---

**Com. Maranga:** (interjection) 1776

**DO:** It came before that, 1780 something. Lakini haijawai kurekebisha mpaka wa leo. Pengine ni kitu kama 30 amendments so ni nzuri kutengeneza kitu ya udumu na ukiangangalia kama America wanasema every vote of....., every vote of .....ndio wanaabisha Rais, and they have been doing that for how many years? Miaka nyingi sana. So, ni nzuri tutengeneze Katiba yetu iwe nzuri sana in a very good way. Sawa sawa? Nafikiria Commissioner ataambia nyinyi mambo mengine, pengine yeye ako na utaratibu yake na hii si kazi ya provincial administration. Yetu ni kukaribisha nyinyi, provide security na

tuone kila kitu inaenda bila wasi wasi. Kwa hayo machache Bwana Commissioner, nasema asante sana. Karibu.

**Com. Maranga:** Asante Bwana DO, watu wa upande ya Shinyalu upande wa Ileho, mimi nawakaribisha kabisa katika hii kikao cha Marekebisha ya Katiba na sasa nataka kutangaza hii ni mukutano wa Tume wa Kurekebisha Katiba na sasa hii mukutano ni rasmi kabisa na yoyote ambayo anatoa maoni hapa hata toa chini ya hiyo sheria ya Tume ya Kurekebisha Katiba. Kabla sija endelea mbele ningetaka kuwajulisha ni akina nani wako hapa.

Ninatarajia ma-Commissioners wawili lakini moja hawezi akafika mwingine namutaraji Dr. Githu Muigai sijui kama anaweza akafika lakini Commissioner Nancy Baraza jana alisafiri hadi Nairobi kwa sababu kuna maneno ingine ya Commission ambaye ilikua urgent ambaye alikua anatakiwa kushugulikia. Kwa hivyo, yule na subiri Bwana Muigai mimi nitazidi na kipindi cha siku ya leo na nataka kuhakikishia kua hata muniona nimeketi hapa peke yangu maoni yenu yatafika katika Tume ya Kurekebisha Katiba na kwanza kabisa hebu niwajulishe ni akina nani tuko hapa na hawa.

Tuko na Programme Officer wetu ambaye anaitwa Fatuma Issa Jama, huyo ndio anahusika na maneno ya Secretariat, kama kuna chochote ambao unataka kuuliza kuhusu Tume ya Kurekebisha Katiba basi huyo ndio mwenye kuuliza. Ya pili, tunayo Mr. Wambeyi Makomere ambayo ni Assistant Programme Officer, vile vile tuko na hule ananasa sauti zenu ambaye anaitwa Mary Babu. Mary Babu ndiy mwenye kunaza sauti zenu kuhakikisha ya kua tumechukua maoni yetu, hata usipoona mimi nikiandika kila kitu ni kwa sababu tuna recorder ambaye ina-record kila kitu kwa hivyo, na hii report badaye mutapata kama watu wa Shinyalu.

Mimi ambaye leo ndio nakaa katika hiki kiao ya Kurekebisha Katiba, mimi naitwa Doctor Charles Maranga Bagwasi mimi ni Commissioner. Na kwa hivyo mimi nataka vile vile kuwaelezea kidogo kwa ufupi masharti ambayo sisi tutafuata.

Kwanza kabisa mtu anayetaka kuongea mbele ya Tume ya Kurekebisha Katiba tuna form hapa. Ukiingia hapa umeona mahali kuna meza hapo nje tunauliza watu wajiandikishe. Sisi tunafuatanga list vile watu wamefika hiyo orona ndio sisi tunafuata na unaweza ukaonyesha ya kua unataka kuzungumuza ama hutaki ama unataka kua observer. Kwa hivyo kuna njia tatu ya kutoa maoni. Ya kwanza kabisa, unaweza fika mbele ya Tume utoe memorandum kwa Fatuma, you register kama unaharaka unaweza ukaondoka hiyo maoni yako imefika kwa Tume. Ya pili, unaweza kua na memorandum lakini unataka kuhusia hile points muhimu vile Bwana DO amesema unatakiwa watu wawe kwa ufupi mapendekezo ndio tuna tarajia sana kwa hivyo mtu anaweza akatoa mapendekezo fupi ya kusema hii memorandum yetu imehusia hapa na pale. Hatuwezi kwa mfano, kama umeandika memorandum tukubalie wewe usome memorandum yote haina maana yoyote, inatakiwa utuambie zile points za muhimu ambayo iko kwa memorandum sisi kama wana-Tume tutasoma hiyo memorandum itachapishwo kama reporti na hiyo reporti itafika hapa Shinyalu baadye.

Kwa hivyo, usiwe na wasiwaisi ati oh mimi sija soma memorandum yangu mbele ya Tume, utupe ile maoni ya muhimu. Kwa

hivyo hiyo ndio njia ya pili ya kutoa maoni. Ya tatu, unaweza kua huna memorandum unafika mbele ya Tume naunatoa maoni yako bila kusoma kitu chochote. Unatoa maoni yako kutoka kwa kichwa chako unasema mimi kama mama ama fulani mimi hii ndio maoni yangu, basi hiyo ndio njia ya tatu ya kutoa maoni na vile vile, unakubaliwa ukuje uketi ndani hapa kwa kikao chetu usikize vile wengine wanaongea, sio lazima utoe maoni na ukisikia fulani ametoa maoni yako yote unahaki ya kusema ninkikuita useme mimi sitaki kuongea na fikiri maoni yangu yamefanya nini? Yamesha tolewa. Tunaelewana?

Kwa hivyo hiyo ni haki yako. Sisi tutakubaliana muda ule ambao sisi tunapeana. Kwa mfano, kama mtu anapeana memorandum na anataka kuguzia maneno ya muhimu, sisi tunampa yeye dakika tatu. Yule ambaye hajaandika chochote tunampa dakika tano. Kwa hivyo usifikiri hiyo dakika tatu ni chache, wacha nikueleze ya kua tumefika Kenya yote mzima hii ndio mukoa wa mwisho sisi tumefika kama Tume ya Kurekebisha Katiba watu wanatoa maoni hata baada ya hiyo dakika tatu hata hawana njia ingine ya kuendelea mbele wanasema tumemaliza kwa hivyo, na mimi kama Mwenyekiti ningetaka mutie hiyo sheria ili tufuate utaratibu bora.

Na baada wewe kutoa maoni hapa ukifika mbele ya Tume kwanza kabisa unajitambulisha majina yako kamili, kwa mfano mtu wakawanza hapa anaitwa Ernest W. Shimenga, nikiita Shimenga atafika mbele ya hapa atajitambuisha tena ile tufanye recordi kwa sababu tunataka tujue hii report ilitokana na nani. Tunaelewana? Ndio hata wewe ukiangalia kwa hiyo report ikija Shinyalu unasema mimi nilizungumuza kumbe nilizungumuza maneno ya muhimu. Kwa hivyo wakati unazungumuza hapa jua hii ni wakati wa historia katika nchi hii usije ukaonekana wewe ndio ulitoa maoni hayana muelekeo utoe maoni ambayo yatasaidia wananchi wa Kenya, watoto wako, vijuku na vituku. Tunaelewana? Kwa hivyo hiyo ni kazi ya muhimu.

Na baada ya wewe kutoa maoni sisi kama wana-Tume tunahaki ya kukuliza maswali, tunaweza tukakuliza swali fulani unafikiria nini, maana ya kukuliza wewe swali si ati tuna weka wewe courtini, hapana, tunakuuliza tu ili tuweze tukajua ulikua unafikiria nini. Kwa mfano ukisema Rais nilazima awe mtu kijana, sasa unajua jina kijana hatuwezi tukajua ni miaka mingapi kwa hivyo mimi kama mwana Tume naweza nikakuliza wewe unafikiria kijana awe miaka mingapi. Tumelewana? Kwa hivyo hiyo ndio maneno ya kuhakikishia ya kua unamainisha nini. Kwa hivyo hiyo ndio nafikiri, na baada ya kumaliza utarudi kwa Fatuma uweke sahihi kitabu chetu rasmi ya kuonyesha ya kua umefika mbele ya Tume ya Kurekebisha nini? Katiba.

Hiyo ndiyo utaratibu wa kutoa maoni. Kitu ingine ningetaka kuwakumbusha ni ya kua kama unamalalamiko kwa DO, kwa Offisi ya Rais, kwa PC, kwa Chief, kwa Assistant Chief hapana kuja hapa uanze kutaja ati DO jina fulani, kama sasa huyu anitwa Bwana Rono ati unanza kusema hule DO anitwa Rono siku ingine aliniweka ndani bila sababu yoyote, hapana taja jina taja Offisi ya DO. Offisi ya nini? Ya DO, kama unataja Offisi ya Chief hapana sema ule mzee wa nyumbani ambaye anakaa Chief ama Assistant ndiyo unataja fulani huyo tunakosana na yeye sana ametusumbua sana kwa sababu ya maneno, hapana taja jina yake sema mimi ni offisi ya Assistant Chief ama Chief ninataka iwe namna hii. Tuemelewana? Na kama ni mwalimu mkuu wa shule ni hivo hivo, kama ni Rais hapana taja jina lake unataja jina ya offisi Offici ya Rais, kama ni Mbunge hapana taja Mbunge wako taja offisi ya Mbunge. Tunaelewana?

Basi, hiyo ndiyo itakua mzuri tusije tukapata maneno, kwa hivyo kutaja majina ya watu hata kama mtu alikua Chairman ya Cooperative Society akaiba pesa ya society yenu upande sema kwa mufano fulani aliibia sisi pesa fulani anitwa fulani fulani ati anaitwa maybe Schivachi ama nini, hapana, wewe unasema hawa watu ambaye wanaibia sisi pesa ya cooperative tutafanyaje na utupe mapendekezo. Tume elewana? Na mimi hapa kama mwana-Tume mimi nataka mutu patie mapendekezo. Kama unasema elimu iko kali iko bei nini, unatakaje? Unataka elimu ya bure ama nini utuwambie hivo hivo kwa ufupi, kama ni maneno ya matibabu hivo hivo, hapana sema tu tabu zako kama mukulima na usipendekeze, fanya nini? Mapendekezo na kwa ufupi tu. Tume elewana? Haya. Basi nafikiri tumesikizana na mtu wa kwanza kabisa anaitwa ni Ernest Shimenga. Basi karibu sasa uje utoe maoni.

**Ernest Shimenga: (inaudible)**

**Com. Maranga:** Well, the way you want, I have given you three minutes it is you people who will decide how you summarize. Na huyu naye vile vile amefanya registration? Anaitwa nani? Secretary naye ameji---

**Ernest Shimenga:** nilikua nimefanya James Mlaga.

**Com. Maranga:** Okay, wacha nione, James nani? James Mulaga. Okay sawa sawa, kwa hivyo sasa nyinyi, wacha kwanza kabla hamujaanza mtu anaweza akaongea lugha yoyote unaweza kuongea lugha ya kimomba, lugha ya Kiswahili, lugha ya mama kama huelewi vizuri lakini sana sana wa-Kenya wengi wanajua lugha ya Kiswahili kwa hivyo munaweza mukaongea Kiswahili ndio DO asikie na mimi nisikie Fatuma na wengineo lakini huelewi hizo lugha bili basi unaweza ukafanya. Na tena kitu ingine wanfunzi wa shule sisi tutawapa special consideration wakati mko tayari nijulishwe halafu nitawaita, alright? Thank you. Anza kwa majina.

**Ernest Shimenga:** Bwana Commissioner, Bwana DO na wananchi wowote ambao tumefika leo, hamujambo? Kwa jina ni Ernest Shimenga.

**James Mlaga:** Bwana Commissioner, Bwana DO na wengine ambao mumekuja, hamujamboni? Kwa majina ni James Mulaga.

**Ernest Shimenga:** Tumekuja mbele ya Marekebisho ya Katiba na tuna memorandum ambayo tutapeana na kwa wakati huu binafsi ningelipenda tuzungumuzia kuhusu preamble. Kwa hile kitabu ambacho tulipewa wakati wa elimu, the Constitution Review Process in Kenya, sitaongea mambo yote ijapokua nita ongea juu ya political na economic powers vile iko ama zime wekwa nchi yetu hii.

Tulionelea, tuna-represent location ya Kambiri na tulionelea vile political power na economic power ziko zaidi kwa either mtu moja political power imewekua kwa mtu moja akiwa Office of the Executive ziwe decentralized ili tuwe na usimamizi kutoka kila pembe ya nchi. Vile vile economic power vile tuko nayo kwa sasa kila kitu tunaelewa kutoka kila pembe ya nchi lazima tuende Nairobi na hizi zikiwekwa kwa kila muko tutakua tunakua na kukua sawa lakini ikiwa tutaweka kila kitu Nairobi ama kwa Office of the President inaonekana tuko pale pale tu ikiwa ni kuandikwa ni mtu mmoja huyo huyo tu, ikiwa ni kuvutwa ni mtu mmoja huyo huyo tu halafu baadaye utakuta wengine wamendela sana na watu wengine wanabaki nyuma.

Ikiwa ni mambo ya economics utakuta headquarter hata ya miwa sisi wenykulima miwa pande hii offisi headquarter iko Nairobi na tukitaka kufuatilia jambo fulani lazima tutafute pesa tuende ku-spend Nairobi na hakuna wakati mtu ya Nairobi ambayo hajui mambo ya miwa atakuja ku-spend pesa yake pande tunalima miwa ama mahali tunavua samaki. So, tulionelea ya kwamba haya yote ya shambaziwe kwa nchi hizo economic power na political power tumeiweka ka maandishi.

Vile vile tuliangalia mambo ya elimu, elimu wakati baba zetu wale ambao walipigania uhuru walipigania uhuru kwa sababu walitaka wa-Kenya waelemishwe lakini tumefika mahali ambapo elimu si bure vile ilikua. Elimu haswa ya primary, Std. 1, Std. 8 tulionelea iwe bure mambo ya malipo mengine, building, serikali isimamie hizo.

Na mambo ya health vile vile tuliona sharti watu wawe wazima ndiyo wawe na uwezo ya kufanya kazi. Ikiwa sasa hospitali zetu wakati huu hakuna hospitali utaende utibiwe bure hata dakatari kukuangalia sharti uwe umetoa pesa na wa-Kenya wengi isijapokua wale wako na vibarua hawana pesa kwa hivyo utakuta wa-Kenya wanakufa kwa wingi kwa sababu ya high costs, so tulionelea hizo ziondolewe na watu watibiwe free vile wazee wetu walipigania uhuru. Ni hayo tu ndiyo naweza ku-highlight na zingine tuliangalia kwa preamble na tukafanya directive principles of state policy na Constitution supremacy halafu citizenship na Defence and National Security.

**Com. Maranga:** Asante, kitu ningekuliza swali moja, unasema unataka political and economic power iwe divorced to the provinces, ungetaka akina nani wasimamia kwa mfano political power kwa provinces, sana sana political power. Kwa mfano kwa provinces tuko na provincial administration, tuko vile vile na county council ni gani ungetaka isimamie?

**Ernest Shimenga:** Vile tuliangalia kwa kikundi chetu tulionelea, yani political power yote imewekua katika Offisi ya Rais na ingelikua ni vizuri Rais awachilie zingine ziwe kwa Parliament halafu vitu kama Ministries zingine zitawanywe ziwe kwa provinces ili tukiwa kama Ministry tatu Western Kenya na Ministry tatu Coast, Ministry tatu North Eastern at least tutakua tunaguza nchi yetu sawa sawa.

**Com. Maranga:** Okay, thank you very much. Nashukuru kwa maoni yenu kwa hivyo naomba muweke sign kitabu chetu rasmi halafu mutupatie hiyo memorandum. Thank you very much. Anayefuata ni Josphat Majanja. Atafuatiua na Tom Shivachi. Tom ako? You will be next. Proceed. Unanza kwa majina.



**Josephat Majanja:** Lira bananganga Josephat Majanja Namusende. .

**Com. Maranga:** Ngoja kidogo huyu atatrafisiri. Yani simama na karibu na mahali ako.

**Translator:** mimi naitwa Josephat Majanja.

**Josephat Majanja:** Bacheni befu boshi mulembe boshi mirembe handi

**Translator:** Wageni wetu wote namusalimu, hamujambo?

**Josephat Majanja:** Maoni kanje

**Translator:** Maoni yangu.

**Josephat Majanja:** Mbola endi

**Translator:** Na sema hivi.

**Josephat Majanja:** Ndikombaga

**Translator:** Na tamani sana.

**Josephat Majanja:** Serikali nianza

**Translator:** Serikali ikipenda.

**Josephat Majanja:** Irisubule malwa ko lutseshe

**Translator:** Itukubalie ulevi au kunya pombe ya kienyeji.

**Josephat Majanja:** Kolutseshe

**Translator:** Ile ya kienyeji ile ambaye ilikua inatumika na murija.

**Josephat Majanja:** Lia khabiri

**Translator:** Kitu cha pili.

**Josephat Majanja:** Mbomba serikali

**Translator:** Naomba serikali.

**Josephat Majanja:** Ikhubekeho muliro kwefu kwo

**Translator:** Itusaidie itukubalie msitu wetu huu.

**Josephat Majanja:** Khwayakho mutsing'ombe

**Translator:** Tue tukilisha ngombe zetu pale.

**Josephat Majanja:** Nukhunyole sikhwina makhono

**Translator:** Nakupata kuni ambazo ziko tayari tusiharibu miti lakini tupate kuni.

**Josephat Majanja:** Mbara kenako niko kandinako

**Translator:** Hayo ndiyo ninaio.

**Com. Maranga:** Mwambie asante sana.

**Translator:** Asante sana.

**Tom Shivachi:** I do not know whether I can put it in English.

**Com. Maranga:** Whichever way, sasa wewe ndiyo utaamua, you can talk in English, Kiswahili.

**Tom. Shivachi:** Nataka nizungumuze kuhusu mambo fulani labda nitatumia Kiswahili ili wengine hawaelewi msikie. Kitu cha kwanza, nataka katiba yetu mwanzo ya Katiba yetu, oh sorry, na jina yangu ni Tom Shivachi mimi ni mwenye kamati wa kamati yetu ya Constituency Constitutional Review Committee. Kwanza langu la kwanza nikwamba katika mwanzo ya Katiba yetu tuweke vitu kama vitatu kuonyesha ya kwamba tumefanya kitu, kitu cha kwanza nataka Katiba iandikwe na watu wa Kenya iwe kwa matumizi ya watu wa Kenya na iwe ya watu wa Kenya, by the people for the people and the people. Nataka hayo yawekwe kwa ile mwanzo ya Katiba.

Kitu cha pili ni kwamba nataka tukumbuke Mungu katika Katiba iseme ya kwamba kwa matumizi au kwa kazi ya mungu aliyumba mbingu na dunia na wote wa diomo, in the service of the Lord the almighty God, the Creator of Heaven and Earth.

Kitu cha tatu, nataka iwe ya kwamba ni Katiba ya maendeleo ambayo itakua Katiba ya haki kwa mapendeleo ya wananchi wa Kenya, for the prosperity of the people of Kenya and just welfare of the people. Hiyo ni upande wa utangulizi wa Katiba. Nitataja kitu kuhusu elimu.

Mimi najua elimu ni kitu muhimu sana, nataka elimu ya shule za msingi shule za secondary zipeanwe na serikali wananchi hawana pesa hizo za kulipa karo elimu ya University, yani the colleges and University iwe supported by Government as it was before. I was in the University of Nairobi some years back and we had some money which was been given to the students and therefore wananchi hawatawza shillingi elfu mia bili kwa mwaka kusomesha watoto wao.

Kitu cha tatu upande wa afya, vile Mzee Jomo Kenyatta alianzisha serikali na akaleta matibabu ya bure sijui ni nani alienda kuharibu, ule mtu ambaye alienda kuharibu mpango huo sijui tuseme nini, basi tunaona watu wapate matibabu ya bure katika hospitali, madawa yapatikane kwa mpango wa serikali na watu wawe na nguvu ya kufanya kazi.

Upande wa ukulima naona ya kwamba vifaa vya ukulima visiwe bei kali sana yani vitu ambavyo vinahusika na ukulima visiwe bei kali sana yani vitu ambavyo vinahusika na ukulima viletwe katika nchi hii bila tax yani vitu kama bolea, mahindi ambayo inatoka hapa Kitale, sijui ni kwa nini vitu hizi vinakua vikali na hawa wazee hawawezi ku-manage, so, all agricultural things should be duty free or should be cheap in order to improve our agricultural production.

Kitu cha tatu ni kuhusu the security. Yani ulinzi ya wananchi. Nchi hii imekua na maafa mengi sana kitu cha kwanza sitaki hiki kitu cha clashes kuaanza kua kwa katika nchi hii. Mtu ambaye atanzisha mambo ya watu kupigana kwa ukabila huyo mtu astakiwe sawa sawa kwa sababu sisi watu wa Kenya lazima tuishi kwa amani. So, clashes ambazo zilifanyika hapa 1990, 1991 and 1997 have completely spoiled our image kwa hivyo mtu yoyote ambayo atapanga hayo mambo akiwa mwanasiasa awe ni nani huyo mtu sheria lazima imuchukulie sawa sawa.

Kitu cha pili, watu wetu asa Police Officers wako tayari sana kupiga mtu risasi. Now, this security element is becoming disturbing kwa sababu unaangalia hata maneno ambaye inafanyika mwana mufunzi anatembea huko Police anapiga yeye risasi mimi nataka Policemen wasiwe na marisasi, life in their guns, let them just walk with those things because they do not know how to handle them.

Kitu cha mwisho labda ni kuhusu hali hii ya Mungu, nitazungumzia mambo ya Mungu kwa sababu bila Mungu sisi hatuwezi kuishi. Mambo ya Commission ya devil worshipping lazima itolewe watu wasikie hiki kitu kilikua nini. Kitu cha pili, lazima sheria ipeane ukweli au mwongozo katika hali ya kuabudu hatuwezi kubali watu ambaye wanchinja watoto wanachukua masikio na vitu vyo wanasema wanaabudu, that is what we mean is the Constitution must be in such a way that the true worshipping should be there not just a general saying anybody is free to worship halafu wengine wana-worship manyoka wengine wana-worship ngombe na huku wanaua wengine ati wanafanya worshipping. So at the style of worshipping there must be the true God who made everybody, let people worship them through any other direction but let the God Almighty be the one who will be allowed to be worshipped.

Ya mwisho ningependa ya kwamba Kamati hii ya Constituency Committee ibaki, kamati ya coordinator ibaki, offisi ya

coordinator ibaki, offisi ya Secretariat in Nairobi ibaki, wakati hii Constitution itakua imesha andikua imekwisha hizo offisi tatu zibaki ata kwa miaka mengine mitano ili wakati wazee hao watukua na mambo ya kuuliza kama sheria walipitisha zinafanya kazi sisi tunaweza itana haraka tuchunguze ni nini kilifanyika kwa sababu ikiwa dismantelled sasa mtu mwingine atachukua hiyo Constitution aweke kwa Attorney General na atakalia kwa hivyo I suggest that when the Commission finishes its work these three offices should remain at least for a time until all the Constitutional things are done.

Na mwisho nitasema ya kwamba Ministries ambazo zinachaguliwa katika nchi hii hazichaguliwi vizuri inachaguliwa kwa njia ya ukabila na nataka Parliament iwe na uwezo ya kuangalia ni Ministries gani ambayo zinatakikana na ziwe distributed for the welfare of the people by qualified people. Thank you very much.

**Com. Maranga:** Asante Bwana Shivachi asante, lakini ningetaka kukujulisha ya kua wahindu wanaabudu ngombe saa ingine kwa hivyo nikazi ngumu sana, ukienda India useme hivo pengine utakua kinyume ya matako yao lakini asante, hiyo ni maoni yako.

Yule anayefuata sasa ni Julius Milimu. Atafwatiwa ni Kipchumba unataka kuongea, Ruto? You want to say something? Brief, okay sawa. Milimu.

**Julius Milimu:** Bwana Commissioner na wengine namusalimu wote, kwa majina ni Julius milimu. Ningelipenda kukuguzia sehemu tatu, administration, forest na education.

Kwana nianzia kwa administration. Mimi ningelipenda mtu kama Assistant Chief, Chief wawe wakichaguliwa na wananchi na wawe wakipata transfer waende wakifanyako kazi sehemu zengine na wapewe muda wakufanya uchaguzi kama ni miaka tano, kama ni miaka tatu wawe wakichaguliwa na wananchi. Hapo nimemaliza hivo.

Kufwatana na forest, mimi ningeliomba serikali irudishe mambo ya forest kwa wananchi kwa sababu mwananchi ambao anaishi kwa forest ndie anajua vile anaweza kulinda msitu yetu hii. Watu ambaye wanalete wizi kwa forest ni watu ambaye serikali inaajilia kwa sababu analeta mtu ambaye hajui mambo ya forest na huyu anakuja anachukuwa wananchi wanaenda kutengenezea makaa kwa forest ama mbao, anafaidika hapa amapata mshahara kwa serikali tena pia anaharibu msitu wa serikali. Sasa inafa serikali irudishe mambo ya forest kwa mwananchi watengenze Committee zao za kulinda forest. Nimemaliza hapo.

Narudi kwa elimu. Elimu ningelipenda serikali ipeane masomo ya bure kwa darasa la kwanza hadi la nane ili watoto wetu wapate hiyo elimu na mambo ya kutoa kiboko kwa shule mimi ningeliomba serikali discipline lazima iwe kwa shule kwa sababu mtoto asipopigwa na mwalimu hawezi akajua kitu ma sisi wazazi tunapendelea kwa sababu mtoto sisi tunashindwa na watoto nyumbani. Akiwa kwa shule mwalimu nido huu anamutengeneza akuje kwa line kidogo. Ni hayo...

**Com. Maranga:** Unasoma magazeti saa ingine walimu wakichapa watoto kiboko wengine wanakufa, wengine wanaumizwa, na unajua hiyo inaenda kinyume ya haki za kibinadamu za watoto, International Convention for the Childrens Rights, sasa utafanyaje?

**Julius Milimu:** Bwana Commissioner, mwalimu ambaye anapiga mtoto anaua huyo ni magaidi kwa sababu mtoto wako ukichapa kiboko ya kumuonyesha amefanya hii makosa hiyo siku muua sasa ule ambayo anapiga mtoto anaua huyo ni magaidi na anafaa achukuliwa sheria ya serikali. Asante.

**Com. Maranga:** Asante ni maoni yako, tupatie hiyo memorandum nauweke sahihi. Bwana Ruto. Unaanza kwa majina yako kamili.

**Kipchumba Ruto:** My name is Kipchumba Ruto ambaye nitato maoni in my privat capacity as a citizen of this Republic but not as a DO. Kwanza kabisa ningependa kutoa maoni juu ya the three organs of Government that is Legislature, the Executive and the Judiciary. That in our Constitution we should have a clear separation of powers so that the Executive should be purely Executive so that Ministers or Assistant Ministers amamanaibu wa mawaziri wasiwe waBunge. They should be purely, ama member wa Executive lakini wasiwe waBunge na waBunge wawe kwa waBunge wasiwe ni members of the Executive.

The Judiciary, mahakama lazimai iwe independent and free na mtu yoyote asiwe, ukiangalia waziri utakuta waziri ni Mbunge yeye ni member wa Bunge lakini ukiangalia vile vile waziri ni member wa Executive so asifanye hiyo kazi so mtu yoyote asiwe anafanya kazi ya ubunge vile vile asiwe anafanya kazi ya Executive. Tunasema mtu moja na kazi moja naikiwa kuna shida kati ya the three organs of the Government they should be equal in power wewe sawa isiwe Executive iko na nguvu kuliko Parliament ama Parliament iwe na nguvu kuliko Executive ama Judiciary so lazima iwe na checks and balances na tunasema ikiwa kuna shida ama jambo ambalo lina husu taifa nzima kwa kingereza tunasema a matter or a general matter of general importance or an important matter which is very important across the country, it should be subjected to Referendum, wananchi wote Kenya waamue kwa kura si kura ya Rais ama kura ya Ubunge wananchi wote waamue. Kwa mfano, wakati wakuondoa Section 2(a) katika Katiba ilichukua muda mrefu sana mpaka ikalete tension lakini siku moja iliambuliwa na chama lakini kama ingetupiliwa wananchi waamu ingechukua maybe siku chache na ingekua nzuri sana so jambo lolote linahusu taifa nzima lazima ipigwe kura ama referendum wananchi wote ndio wata piga kura.

Police, idhara ya Police. Wamepewa jukumu kubwa ma wako na uwezo kulingana na sheria, sheria ambazo ni mingi na Police wanapo itekeleza kazi yao hakuna mtu ambayo wana-supervise Police hao ni Police lakini juu hakuna mtu ambaye ana-supervise. Tunasema tunataka Police wale ambao wana-supervise Police wengine ama any other authority ambao wata-supervise Police kwa sababu wananchi wanalia sana, utakuta wameshikua huko msituni wakafanya Kangaroo court wakienda ku-complain wanaenda kupeleka the same, same report kwa yule Police mwenyealie fanya Kangaroo court so huyo

mwananchi hatapata haki. Mapolice wako na sheria nyingi sana so wengine wanapotosha sheria so tunataka proper supervision from another organ of the Police to supervise or any authority to supervise the Police so that they can not render injustices to the members of the citizens.

Offisi ya Ombudsman hiyo nikuangalia mambo ambayo yana shida za wananchi, ikiwa haijatekelezwa na DO, mwananchi ako na fursa ya kwenda kumulalamikia amakupeleka malalamiko yake kwa offisi ya Ombudsman. Jukumu ya Ombudsman ni ku uliza idhara ambayo huyo officer anafanya kazi aulize kwa nini huyo officer hajafanya hiyo kazi. Ukiangalia nchi zingine wako na hiyo offisi, ukiangalia kama Scandinavia and countries kama Norway, Denmark ata Britain wako na Parliamentary Commissioner for Administration. Ukichelewesha unajua unakuja offisi huko inachukwa week moja hata kitambulisho ama unaambiwo shida yako itaangaliwa, utangaliwa, ukirudi mara ya pili bado, bado tunaangalia inatakiwa iwe very effective and efficient na ukichelewesha mi jambo ambalo tunaita mal-administration si jambo nzuri so kwa Katiba tunaomba ama ninaomba kama ni maoni yangu ya kwamba iwekwe kwa Katiba na hii offisi lazima, ama tunasema iwekwe kwa Katiba. Na mwenye atakwa Ombudsman Kenya lazima ni mtu of high integrity, must be educated, must also be a person who is concerned with the citizens of the republic and fair administration in the country.

Jambo lingine nikuhusu appointments, wale ambao wanateuliwa kuchukwa jukumu---

Because mtu anaweza kua mwizi leo kesho ndio anasimamia pesa nayeye anjulikana ni mwizi manaa anajua. We have seen people wakati wa.....na mimi natoa hii as a private citizen of this country, mtu ana-grab shamba ama beach plot kule Coast ama Pwani anataka million hamsini anakuja kwa wananchi anambia sasa kwa sababu ya wizi yangu na niko na pesa sasa niniataka niwe Mbunge si analeta hizo pesa hapa anakuja kufanya harambee mwishowe mutachagua yeye awe ni Mbunge na akifika Parliament sasa atakua yeye ni waziri. Wewe ni mtu mzuri katika nchi hii kweli? Sijui, sitakai niulize nyinyi maswali lakini mara kwa mara inatendeka namna hiyo so any appointment should be subjected to Parliamentary scrutiny ikiwa mtu atafanya kazi kwa njia nzuri ama hapana.

Public Accounts Committee katika Parliament. Mara kwa mara wana-record matumizi ya pesa ya serikali wakati ambazo hizo pesa zimetumiwa na ni maramoja kwa mwaka tuseme hili kukinga ama kuchunga hizo pesa isitumiwe kwa njia ilio mbaya ama njia ambaye si nzuri ni sharti watoe reporti yao mara mbili kwa mwaka so that they can rectify the department kama wame misuse hizo pesa. They can rectify so that in the next part of the financial year they should be able to do something or save some money so that it can not be wasted.

Parliament ama mbunge maoni yangu iwe mara mbili tuwe na house of representatives aliyo lazima ichaguliwe na wananchi kama sasa na tunaomba ama naomba House of Senate kama ile House of Lords ya wingereza na hii ni lazima ama wachaguliwe kulingana na mikoa na hi House of Senate kama ile kabla ya uhuru ama baadaye ya uhuru lazima iwe na checks and balances so that they can control each other hii ikitaka kuongeza msharha ya MP hii chumba lingine inasema hapana so that wapewe special

duties so that they can control the other one lakini House of Representatives ndio watachaguliwa na wananchi House of Senate kulingana na mikoa. Pengine wawili wawili ama kila district moja moja ama wawili wawili kutoka district.

Maoni yangu kuhusu sheria ya Kenya za Kenya ukiangalia sheria za Kenya from independence hawajawai kufanyia marekebisho ni kama Katiba for a very long time some of the laws of this country they are obsolete hawaja rekebisha ni kama hii Katiba ya Kenya sasa, hawajawai kurekebisha mpaka wa leo hata tunawapo kutekeleza kazi yetu ni shida sana utakuta mtu 63 inasema kupatikana na changaa kuenda courtini ni jukumu la kimwi kusema utatoeshwa shilling tano..... na litre moja ya chaanga mpaka wa leo the same same Magistrate bado wanatumia hiyo sheria shillingi tano ya 63 na shilling tano ya leo ikotafauti sana na hiyo sheria tunasema zirekebisha.

Haki za binadamu should be protected, should be respected and should be entrenched in the Consitution.

Mwisho, nasema the wishes of the majority in this country utakuta kabila ingine iko kubwa ingine ni wachache so the wishes of the majority should prevail but the interests of the minority should be also protected in the Consitution. Kwa hayo machache nasema asante sana.

**Com. Maranga:** I have a question. I am very keen on the Police Department, are you happy the way the Police is today? For example you have Administration Police, Kenya Police, Stock Theft Unit, GSU and so on, what can you give as a way forward? Because we have had a lot of complaints from mwananchi I want to hear from your own point of view.

**Kipchumba Ruto:** From my experience as in the provincial administration training wanapata kwa njia iliyo nzuri sana sheria wanafundishwa ya kutosha but when they come down to the people at least the .....they are in a better position to those tunaweza ku-control hawa even the Police but now when they are alone wanapo teleleza kazi yao tunapo watuma waende inje utakuta yeye huyo officer na mwananchi so hawafanyi kazi kwa njia ilio nzuri, sio wote wachache ndio wanaharibu lakini majority wanafanya kazi lakini inatakiwa proper supervision and to add on that mimi nasema this officer is arresting officer anapeleka wewe kwa kituo cha Police ukifika mahakamani they are also the prosecuting officer wanafanya kazi mbili mtu moja.

So, kwa kuongeza na hiyo ninasema ama maoni yangu ni that the Police should not arrest and go and prosecute. Mwenye ana-prosecute should be independent body, the prosecution service Commission, we should have a prosecution service Commission so that we de-link to Police from arresting and prosecution so we should have another department.

**Com. Maranga:** The last question, how can we for example control false accusation by the Police because most wananchi what they have said, somebody will be arrested maybe he was trying to take kuni from the forest but when the Police Officer feels that is not good enough anamuwekea changaa mtu anawekewa changaa pengine ni Reverend or he is an elder in the village. How do we, because that is really been a very serious complaint.

**Kipchumba Ruto:** Hiyo, that is why nilisema tuwe na hile offisi ya Ombudsman, tuwe na hiyo offisi ya Ombudsman atakua ana-inquire then ya pili nimesema wale ambayo wana-prosecute should be independent from the Police iwe a different department altogether.

**Com. Maranga:** That one I agree with that.

**Kipchumba Ruto:** Yes. Thank you.

**Com. Maranga:** Thank you very much Bwana DO, please sign our official register and give us that memorandum. Thank you for your good views. Now niite wanafunzi wa Chandarima Secondary School, sijui niwangapi kwa sababu majina yao sioni so can we have them, the order they are going to come. How many are you? Two, there are three of you? Okay, so I think you can present one after the other, you start with your names you tell me the school and the Form you are in okay? Good.

**Ogada Perminus:** We are three but I am the one to present.

**Com. Maranga:** The two are not talking?

**Ogada Perminus:** They will just say their names. My names are Ogada perminus in Form 2.

**Com. Maranga:** Okay, let me have the other ones.

**Joshua Ligavo:** Nawasalimu nyote hamujambo? Kwa majina ni Joshua Ligavo mwanafunzi wa Chandarima.

**Com. Maranga:** Any Form?

**Joshua Ligavo:** In Form Four.

Nawalimu nyote, hamujambo? Kwa majina ni Evelyn Fatenje from Chandarima Secondary School, Form Four.

**Ogada Perminus:** I will present the news then I translate it into Kiswahili.

**Com. Maranga:** You can present them in any way there is no problem.

**Ogada Prerminus:** Suggestions; The Government should establish a Commission that shall be charged with the responsibility



of disasters, e.g. floods. When there are flood it is when the Government is coming in to establish a Commission to deal with it, they must just establish it earlier to deal with such cases. The Commission should get its share of funds from the Exchequer of this fiscal year.

A question on Constitution. How will the new Constitution ensure that the recommendations of Commission set by the Government are followed? Second, we do not know how the old Constitution was about so that we are just being told we have a new Constitution so we do not know how to rectify our need, we should have been given out how the old Constitution was headed we can amend the new one.

Then, I will talk about opposition parties. I think we have more than 40 political parties in Kenya but for students like us we just know of KANU which is always just talked about in our mass print everyday and whenever they broadcast their news they are just favouring the political party, so we should have a new Constitution whereby every party will be presenting its views, its future arrangements at least every week so that we can know the..... I think that is all.

**Com. Maranga:** Let me answer the first question, how will the new Constitution be implemented, I think you need to tell us how but what we are supposed to do after collecting the views of Kenyans we are going to collate them, that means that we are going to put them together, after that we will analyze and see what Kenyans have said, after that we are supposed to change the laws of this country. You heard the earlier speaker saying that the laws are obsolete so we want to change the laws in such a way that they can be consistent with the Constitution. For example, if you want to establish a Commission on disaster management then I will put it from the Constitution but that, that kind of Commission needs to be established. How and when and how it will work now that becomes the domain of Parliament, Parliament now through an Act of Parliament will be able to formulate the policies and programmes of that Commission. Are you getting my point?

Why did we not give you the old Constitution? Well, we tried as a Commission given the short period of time we gave people to undertake civic education but that is one of the major problems which we have said that the old Constitution was never accessed by many Kenyans but what we are saying is that the law which established this Commission actually you can ignore the old Constitution in such a way that you give your views so that if they are any sections of the old Constitution which tally with your views that section should remain. Are you getting my point?

So, we said we do not also want to belabour the point but we want to go through the old Constitution and suggest specific amendments. The law which established this Commission is that it is for comprehensive Review of the Constitution, that means Kenyans can decide to come up with a completely new type of Constitution. For example when you say people say we want majimbo, that is not in the current Constitution but it was there in 1963 but that 1963 Constitution was never implemented it was never given a chance, you get my point? So I think you have already given your views and let us hope for the best and thank you very much for appearing can you sign our official register and hand over your memorandum. Then next person

anaitwa, namuitwa sasa Netty N. Mate. Okay, atafuatiwa na Eupharata Musavi, ako? Yes you will be next.

**Netty Mate:** Hamujamboni wote? Mimi kwa majina naitwa Netty Aroso Mate natoka---

Hi maoni yetu tulikua, tulikaa kwa kikundi halafu tukafanya mujadalo halafu tukaandika majibu yake ndiyo mimi naenda kulisoma na tuliandika katika kimombo.

**Com. Maranga:** Nafikiri ungetupa tu kwa ufupi kama ni mrefu tutajie ile main points, tumeelewana? Yani badala ya kusoma memorandum yote uwe unatutajia ile maneno ya muhimu, kwa mfano tulisema preamble tukazungumuzia maneno ya whatever namna hiyo. Tume elewana? Unanielewa?..... Hapana, sasa hiyo kama ni kuuliza majibu na ku-answer hiyo, that one you can hand over to us but if you want to highlight some points you better because hiyo itakua kama wewe unafundisha watu hapa itakua kama mwalimu.

**Netty Mate:** So I should only read the others.

**Com. Maranga:** Just highlight the main points, what did you come up with as your main recommendation. Do not ask that question which we have in the booklet and then you answer it, just give us the highlights that what you have agreed is a,b,c,d.

**Netty Mate:** Sisi tuliandika kuhusu management and use of national resources. Our nation has experienced problems with.....management and distribution of finance and management of human resources. ....controls these powers.

.....namba moja ilikua Parliament to support community participation in management and use of resources. ....tukajibu, yes Parliament should be trained halafu tukajibu foreigners or.....harambees, fund raising through transparently organized .....promotion of income generating activities in .....which can be envisaged in the Constitution is through.....

Jibu ya tano ikawa yes the Government should be required to apportion benefit from resources between the control Government and the community where such resources are found. Jibu ya sita ikawa, we can enhance the role of the Controller and Attorney General by having him appointed thorough Parliament plus having other senior officers know by the public to assist him. Jibu ya saba ikawa, the Parliament should appoint the Controller and Attorney General. Jibu ya nane ikawa, the.....which Parliament can use to control management and use of public finances is the ability to ..... Jibu ya tisa ikawa, in order to attach....Kenyan to work in the .....services they should be.....powers to appoint most of them. Jibu ya kumi ikawa, we can strengthen the management and discipline policy of the Public Service Commission by ....the appointment procedures, e.g., .....Commissioners. Ya kumi na moja ikawa, members of the Public Service Commission should be appointed by the Parliament. Ya kumi na mbili ikawa, .....should be a court of ethnic by ethnic.....in order for them to know that they should also follow..... Ya mwisho, ikawa yes the public officers should be required to declare their .....

**Com. Maranga:** Thank you very much, hand over the memorandum and sign our official register.

**Euphrata Musali:** Kwa majina naitwa Euphrata Musali from Lunyu sub location. Tulikalisha vikundi tukifundisha civic education tukatoa maoni kwa wananchi na tukaandika chini. Our topic was cultural, ethnic and regional diversity and communal rights.

Kenya has a rich diversity of cultures that are not addressed in our Constitution. Number one, Kenyas ethnic and cultural diversity does not contribute to a national culture that is sukuti, in-fighting, alcoholism initiation in brackets circumcision, tooth removal and excetra.

Number two, cultural and ethnic diversity should be protected and promoted by the Constitution like.....and property inheritance. Number three, any Kenyan person should exercise his or her rights to vote. Cutural and ethinc needs within the Republic that is circumcision, female genital mutilation. Number four, I do consider myself as part of a distinct social group who 's interest should be catered for in the Constitution, that is as a Luyha, mukoloko in brakets.

Number five, you mentioned the.....group.....and requirements the groups specific needs and requirements should be adequately addressed e.g. the style of Tiriki circumcision. Number six, ethnicity should be duly recognized and appreciated but noticed in promoting...and patriotism, e.g. it is not wrong to support a Luyha politician if you are Kalenjin and vice versa. Number seven, the Constitution should provide for protection from the discriminatory aspects of culture, e.g. compulsory marriage and forceful marriage. Number eight, we should have more than two national languages, e.g. Kiswahili, English, Mother tongue and any other foreign language which is lingala or any other. Number nine, the Constitution should recognize and promote all indigenou languages. And that is all.

**Com. Maranga:** Let me ask you a question. What did you say about Female Genital Mutilation? Do you want to circumcision of girls to continue or not?

**Eupharata Musali:** If it is there let it be known to natural, if it is there or if someone wants to do it or any tribe let it be known.

**Com. Maranga:** So you have no problem if the Luyha's are doing it they can continue.

**Euparata Musali:** If it is known but not to continue doing it in such a way.

**Com. Maranga:** Okay, thank you very much, asante, sign and give us your memorandum. Edna Sirisia. Karibu, halafu

atafwatiwa ni Erastus Sore, Erastus ako? Okay uwe tayari.

**Edna Sirisia:** Murembe bosu murembe handi

**Translator:** Jambo(inaudible)

**Edna Sirisia:** Nangwa mbu Edna Sirisha

**Translator:** Mimi na itwa Edna Sirisia.

**Edna Sirisia:** Nyanza ndi nilokhobo lilondokhana nangwa President namalire khubakho yakweme yakho maliale serikali kabere kange nangwa khubulakho khukalura khandi khuye tawe khulobolere rero musituwo shindi

**Translator:** Nataka kuaanza na neno ili la....inasema ya kwamba wakati Rais amechaguliwa mara ya kwanza anapofika mahali pake amalize miaka tano inatubidi tena tusimuchagua.

**Edna Sirisia:** Kalolekhanga ndenangwa likhuwa lindi liakhubola ndi endangwa ndibula mwana muyayi.

**Translator:** Nina furaha kwa sababu mimi nimeza kijana.

**Edna Sirisia:** Mwana mweneyo alanyola mulimo

**Translator:** Huyo mtoto atapate shamba

**Edna Sirisia:** Khandi ndebula mwana mukhana

**Translator:** Tena nimeza musichana

**Edna Sirisia:** Mukhana mwene alanyola mulimo

**Translator:** Tena yule musichana apate shamba

**Edna Sirisia:** Khandi mwana mukhana oyio wachalukhale

**Translator:** Tena huyo musichana ameolewa

**Edna Sirisia:** Khumusakhulu wewe

**Translator:** ako bwana yake

**Edna Sirisia:** Mukhana mwene alakhwebwa

**Translator:** huyo musichana atalipiwa mahari

Ya pili, mtu kama ameshikwa kwa nchi yetu ningenelea maoni yangu ya kwamba ingekua karibu kama wangelete courti ama judge wakuje kwa division kufanyia kazi kwa division ingekua vizuri kama mtu ameshikwa na makosa angefanyiwa haraka casi yake kama ni ya kuhukumiwa ahukumiwe makama sio ya kuhukumiwa awachiliwe arudi kwa kazi yake haraka kuliko kupeleka kwa district ndiyo apate kuhukumiwa huko.

Maoni yangu ya tatu watu wanayofanya kuhudumia raia anaanzia kwa sub location na ingefaa Assistant Chief kama amechaguliwa na serikali kwa kupitia kwa njia ya interview na wale watu ambao chama kinacho unda serikali raia ndiyo wanachagua hili mtu kutoka hata kwa sub location, hawa watu wote walipwe mshahara.

**Com. Maranga:** Akina nani unataka walipwe mshahara?

**Peter Kichama:** Kama mtu kama chama ambacho kina----

**Com. Maranga:** (interjection) Kama wewe sasa?

**Peter Kichama:** Kama mimi sasa.

**Com. Maranga:** Oh, Okay.

**Peter Kichama:** Viyombo vya serikali kama magari, misitu, barabara na vitu vingine ambazo vinalete pesa kwa serikali kama bahari hizo vitu pesa zile ambazo zina toka huko kama tuna vyama viwili vile ambavyo vinaendesha nchi hii viama vyote vijue

kazi ya hizo pesa kuliko chama kimoja kutawala hiyo pesa.

Neno langu la mwisho ama---

**Com. Maranga:** Hiyo ndiyo ya mwisho.

**Peter Kichama:** Hiyo ni ya mwisho hiyo mimi naenda kusema. Tue na mali hii ya uma ambayo tuko nayo kama tunaweza kua na shule mahali na hiyo shule itolewa na hiyo shule itolewe halafu hiyo plot inabaki bure empty, hiyo plot kama tuko kwa divisions kama yetu ya Vihiga hii tupatiwe hiyo plot tuna watu wale wanakufa hawana mahali ambapo antawanweza hata kuzikwa tukubaliwe na serekali tutumie plot kama hiyo kuzika hawa watu. Asante sana Bwana Commissioner kwa hayo.

**Com. Maranga:** Bwana, wewe ni KANU Chairman, kuna shule yoyote imefungwa hapa na unataka iwe cemetery?

**Peter Kichama:** Tuna hata makanisa zingine zili weza kufungwa na hiyo viwanja zimebaki bure.

**Com. Maranga:** Imebaki bure? Lakini hiyo makanisa ilikua na title deed?

**Peter Kichama:** Ziko naye.

**Com. Maranga:** Sawa. Asante. Weka sahihi hapo, kuja weka sahihi na upeane memorandum. Abednego, atafuwatiwa na Martin Musonye, Martin Musonye ako? Okay you will be next.

**Abednego Asango:** Basi Bwana Commissioner, wazee, wamama ambao wamefika hapa nawasalimu, hujambo? Mimi kwa majina ni Abednego Asango mimi ni muraia mwema mukazi wa hapa. Niko na mambo ya kusema mawili, matatu.

Jambo la kwanza ni kuhusu vyama vya kisasa. Ningependekeza mbele ya Commission ya kwanza tue na vyama vichache sana, ikiwezekana pengine vyama viwili tu vinatosha. Hii vyama vingine vyote ni kupotesha wananchi but mwishowe tunatoa kiongozi ambaye pengine si popular.

Jambo la pili ni kuhusu serikali ya majimbo, federal Government, federal Government we do not need it at all....serikali ya majimbo kwa sababu serikali ya majimbo inaleta ukabila, tribalism, nepotism, and .....kwa hivyo mambo ya majimbo tukiwa nayo hata kua unity yetu ya Kenya kwa hivyo hapo serikali ya majimbo Bwana Commissioner, mimi natoa maoni yangu nasema siipendeli sana.

Kwa upande wa Legislature Bwana Commissioner, naona ya kwamba the President should appoint Minister, Assistant Minister



and top civil servant only lakini at other appointments as in the case today like judges, Parastatal Chairmen tuwachi Tume fulani kwa sababu tuko na competent people down here who can be appointed by a Commission that because they have not been seen in the eyes of the President they are left suffering down there. Kwa hivyo ningependekeza these other civil servants I mean hata Commissioners kukiwa na Commissioner ambaye unaweza ku-elect watu ambaye wanaweza kujaaza offisi ingine za serkali.

Kuhusu mambo ya mshara ya MP's, MP ni mwananchi kama mimi hapa kwa nini yeye anapewa nafasi ya kusema mambo ya mishahara wake na mimi hapa kama mwalimu sipewi nafasi ya kusema mishahara wangu? Kama sisi wote wana Kenya MP akisema mambo ya mshara kwa Mbunge huko na mimi pia hapa kwa shule ni seme mambo ya mishahara yetu hapa halafu tutakua na usawa otherwise naonelea ni makosa hii nikusema tunalia upande pamoja wengine watu akipata shida.

Tena kwa upande wa MP's, nominated MP's, hawa ambaye wanateuliwa mimi sioni haja na maleta MP unless he is nominated to serve a few kwa sababu kama elected MP's why should he have nominated MP's? Lazima mtu ambaye anaitwa Mbunge ambaye anaenda kupata yule mishahara mnono apate kura ya wananchi kutoka hapo chini lakini hii mambo ya nomination nikuonyesha there is an agenda somewhere hidden ambaye unataka huyu mtu a-support, hiyo sasa kwangu nasema siwezi nikakubali hiyo.

Lingine, President, President should be removed from office if, yafaa Rais atowe kwa offisi kama uchumi wa nchi ni baya kwa sababu kama uchumi wa nchi una yumba yumba like these public...President aendele, aendele, aendele, hapo tunaharibu serikali. Kama yeye pia ako corrupt lazima tuwe na njia ya kusema sasa serikali sio muzuri wewe unatoka kwa offisi, tena kama fikira zake si muzuri....lazima pia atolewe kwa offisi tuone nani anaweza kuendesha serikali na pia asiwe involved kwa scandal ingine mambo ingine ya hapa na pale, nataka akiwa President awe mtu straight. Bwana Commissioner naenda haraka tu.

**Com. Maranga:** Last point.

**Abednego Asango:** Last point but not least. The two year term for Mayors and Chairmen of county council is very short kwa sababu mtu hajaonyesha competence yake. Ningependelea pengine mtu akitaka kua Mayor ama Chairman wa county council apatiwe miaka mitano ili ndiyo aonyeshe nguvu zake ama ujuzi wake hapo.

Na la mwisho ni kuhusu hii death sentence Bwana Commissioner, tumesikia watu amekosa mambo fulani pengine ameuia mtu halafu courti inasema huyo mtu tunataka tumufunge apitie kwa kinyangi anyongwe lakini baada ya miaka kumi tunaona hawa watu wanatembea hapa halafu tunashindwa tulisika huyu mtu yafaa anyongwe, kwa nini tena anatembea hapa? Ati he has been pardoned by the President, if it is life, life must be life for life, why should he curtail somebody's life and then tomorrow you expect to enjoy you own life? Asante sana Bwana Commissioner.

**Com. Maranga:** Asante, na uweke sahihi kituabu chetu rasmi. Martin Musonye halafu atafuatiwa na Constance Shakali, wewe iko? Okay sawa.

**Martin Musonye:** Yangu Bwana Commissioner, nikuhusu good governance in the country. Good governance---

**Com. Maranga: (interjection)** Anza kwa majina.

**Martin Musonye:** Majina yangu ni Bwana Martin Musonye na mimi ni Chairman wa Shinyalu Constituency Constitutional Committee. Maoni yangu ya kwanza ni kujusu good governance. Good governance I am talking of a Government which is transparent, accountable and with a vision. For Kenya's economic growth Bwana Commissioner, we make these ones to be addressed strictly. Bwana Commissioner, nafikiria kua na hayo kufanyika vizuri inatakikana tuwe na judiciary ambayo iko independent na tena nafikiria tuwe na Police force ambayo iko na watu ambayo wame elimika via kutosha na wanaweza kufanya kazi bila mapendeleo.

Accountability inatakikana mtu awe protected legally ili accountability ionekane na inatakikana watu wawe ambao wanaandikwa ambao wasiwe wanajifikiria masilai yao wenyewe.

Law and order Bwana Commissioner, inatakikana kila mtu wote Kenya mtu yoyote awe mdogo awe mukubwa awe protected equally na serikali yetu kisheria.

Fraud; fraud is an economic ill, it is my proposal Bwana Commissioner that we have a clause in the Constitution to state that anybody involved in fraud when it comes to economic issues should be subjected to prison, imprisonment because it is from this juncture or in this case where even investors are always discouraged from investing in our country. We have some institutions like public procurement. Public procurement imeshikwa na ufisaji sana, it is therefore my proposal Bwana Commissioner that the Office of Public Procurement Officer should be empowered and should be a fully fledged office with Secretariat who are properly educated and experienced to be looking into the procurement procedures of public goods and services.

Infrastructural issues Bwana Commissioner, tumekuta kuna ufisaji ambao inatokea wakati watu wanaporekebisha ama kutengenze barabara zetu na tunataka watu ambao wanahusika kwa sababu kila wakati pesa zinalipwa kutengeneza barabara na hizo barabara hazitengenezwi vilivyo kwa hivo tunataka yoyote ambaye anahusika na kutengeneza barabara zetu na anafanya kazi duni astakiwe.

Bwana Commissioner, mambo kuhusu elimu ninamapendekezo ya kwamba elimu ipewe bure kutoka class one mpaka Form two, hapo nafikiria mtu atakua amejimudu kusoma na kuandika. Pia Bwana Commissioner, ni mapendekezo yangu ya kwamba

wasomi wakifika University na wakitoka huko wapewe kazi na serikali wasipopewa kabla serikali kwa sababu ya ukosefu wapewe loan za kuanzisha biashara kidogo.

Bwana Commissioner kuhusu national resources ni mapendekezo yangu ya kwamba kila tribe Kenya iwe considered equally na napendekeza ...ya kwamba national resources iwe based on population. Mambo kuhusu natural resources ni mapendekezo yangu ya kwamba watu ambao wanakaa karibu na natural resources na...msitu waandkiwe kazi ya kulinda hiyo misitu.

Elections, ninapendekeza ya kwamba watu ambao wanafaa kuchaguliwa kua councillors ama Wabunge wawe na minimum qualifications of Form Four na kwa vile nimependekeza decentralization of resources Bwana Commissioner, na pendekeza tena hawa watu wakifika huko na wakose ku-perform they should be recalled within two years.

**Com. Maranga:** Last point.

**Martin Musonye:** Bwana Commissioner, I am talking about children, children should be given free education, basic rights and basic needs and for those who are incapacitated they Government should provide for that.

**Com. Maranga:** Thank you, thank you very much. Now we have Constant Shakali.

**Constant Shakali:** Bwana Commissioner na wengine ambao wako hapa pamoja na wamama na wananchi ambao tunaishi nao hapa, hamujamboni? Hamujambo tena? Mimi maoni yangu Bwana Commissioner, ni kuhusu umaskini ambaye iko kwa sisi na ninawazungumuzia hii upande wa administration.

**Com. Maranga:** Majina sema kwanza.

**Constant Shakali:** Constant Shakali. Upande wa umasikini wetu iko hivi, tangu mwaka wa 1967 wakati ambayo land registration ilikua ikipita hapa hata sisi, hiyo ni maoni yangu tunataka serikali itusaidiye. Wakati huo tulikua bado wajana ni over thirty years now. Sasa sa hii, ukitaka kupata number yako ya shamba yako hata baba yako akitaka kukupatia shamba ni ngumu sana Bwana Commissioner. Kitu ambaye kinakuletea shida lazima uwe na pesa ndiyo hata baba yako akupatie shamba.

Kitu imkuja iko hii lazima uchukue baba yako muende naye kwa courti muende uchukue watu wa.....na nyinyi ni vijana kumi, sasa watu wa .....hao kila mtu anatakiwa elfu tano na mimi sina kazi, hiyo Commissioner, nataka usaidizi hapa. Watu wa land registration warudi baada mwadakano wakuje wale vijana ambao hawajapata mashamba wanapewa kwa sababu iko wale ministries, wameongeza ministries hapa Kenya na ministries hizo, hizo pesa ambayo zinatumiwa kwa hiyo ministry haina kazi. Ukienda kama Ministry of Works wame weka tena Transport and Communication na hawa watu yote wanafanya kazi....

Tafadhali hata warudishe Ministry of Works wa kutengeneza mabarabara watoe maneno ya Transport and Communication na hizo pesa ambayo ziko kwa Transport and communication ziwe za kulipa hao watu ambao watakuja ugawaie hawa watu masharti.

Neno lingine ambao maoni yangu. Tunafinyika, tuko na Ministry of Forests, tuko na Ministry of Administration, tuko na Ministry of Livestock halafu tuko na Ministry of Water Development, huwezi kupata mtu ya Water Development anaenda kuingilia Ministry of Works lakini kwa wakati huu tunataka muturekebishie sasa Ministry of Administration imeingilia Ministry ya pori. Hapo tumeshindwa sasa kila hii wakati ambao yako nyuma, beleni, ilikua mtu kama iko kwa Ministry of Livestock afwatane tu na ministry yake asingilie ministry ya mtu ingine lakini hapa tuko na shida. Unaweza kupata Administration Police wako kwa musitu.

Mtu akienda ati wameiba ngombe hawaendi, wanataka kwa musitu ili ndiyo wapate mtu huko mtu anachoma makaa ama anaiba mbao hata hao ndiyo wanatengenza plan ya kutengeneza mbao ndani halafu wanasema huko watapata posho hiyo tunataka murekebishe.

Neno lingine ni hivi kwa maoni yangu, Assistant Chief anapata report kutoka kwa .....Chief anapata report kutoka kwa Assistant Chief lakini mtu ambayo amebeba mufuko ya hawa watu wote mpaka kwa DO ni mzee wa mtaa na mzee wa mtaa hapati mshahara na yeye ndiyo iko na kazi mingi amejua kwa Samuel, amajua kwa Joshua amejua kwa .....lakini Chief hata kwangu hajui hata DO kwangu hajui na anapata mshahara kwa maneno ambayo mzee wamuta ame---- Mimi naona hii vitu yote mzee wa mtaa apate mshahara. Tena kwa hawa wazee wa mtaa tunataka wamama wa mtaa tuko na ma-case ingine vile ambaye watu waekosania ndani ya nyumba mama wa mtaa hakuwako wakupata hawa wamama mulikimbisha hawa. Na hayo tu, asanteni.

**Com. Maranga:** Asante Bwana Shakali, weka sahahi kitabu chetu. Chales Mbwabi halafu atafuatiwa----

**Charles Mbwabi:** Ma-Commissioner wetu nawahusika wote, hamujambo? Mimi kitu ya kwanza—

**Com. Maranga: (interjection)** Ni majina kamili.

**Charles Mbwabi:** Mimi naitwa Charles Mbawbi...mimi ni Chairman wa party hii Ford Kenya. Mimi kitu ya kwanza nitazungumzia mambo kuhusu hospitali. Mimi nimitoka nimienda kujibiwa kwa hospitali kama Kakamega halfu bahati mbaya mimi nakufia huko, nikikufia huko sasa inaonekana watu yangu jamaa yangu walipe hospitali bill ya hospitali tena kwa motuary mahali ambaye niliwekwa store ya maiti tena walipe huko. Hiyo jambo nikulipa mara mbili, afadhali mtu alipe mara moja kwa hospitali halafu waje wachukue maiti yangu kwa kutoka kwa mortuary. Mtu hawezi akallipa mara mbili na alikua anakufiwa hapo.

Jambo la pili, mimi nasema namna hivi mimi ni mzee nilienda retire na mimi nataka kupumizika au kupoa na wazee wenzangu mimi sioni kwa nini nimienda kupoa huko na wazee wenzangu nakimbishwa bio bio saa ingine mkono imefungika ati mimi nakunyua pombe haramu, ni nani alita pombe hii haramu na kama anaita hii pombe ya busaa haramu na changaa je, pombe yetu ya kienyeji ilienda wapi, huyo mtu atuonyeshe hiyo pombe asilimali ambao tutaenda kukaa tupate freedom to refresh ourselves.

Haya, mimi jambo lingine mimi nazungumuza nikuhusu hii safari ndefu ya President. Unasikia President ametoka anaenda Amerika na amechukua msafala wa watu mingi, hao watu wanenda kufanya nini kwa hiyo mukutano? Baada ya kuchukua mtu moja waende wapitishie kwa mukutano yale wanatarijia warudi sasa ni musafari ya watu wengi haya, wengine wanatanguliwa kule pesa mingi kama hii Presidential Press Unit. Hilo jambo naona kama inamaliza pesa ya Kenya bure.

Jambo lingine, mimi nataka hivi, watu wengi wanenda courtini wakienda courtini, mimi sijui Kizungu, ile magistrate kwanza akiwa magistrite mwanamuke anazungumuza haraka haraka Kingereza yako hiyo mimi sisiki sasa mimi nastukia tu mimi naitika jambo fulani kumbe hilo jambo niliitika, nataka courti tuzungumuze lugha ya mama lugha ya kienyeji, understandable language. Kama Wazungu wanazungumuza Kiluyha huko tena hapa tuzungumuze Kizungu, kama Wazungu hawazungumuze Kiluyha huko sisi hapa tuzungumuze kienyeji courtini na tena court hii ya makosa ndogo ndogo mimi naonelea ikuje .....chini. Pia Chief awe na magistrate wake wa ku-deal na cases ndogo kama ya makaa, hii changaa munaita pombe halafu na ni pombe mzuri ya kienyeji hii.

Halafu kitu ingine, mimi nitazungumua ni kuhusu nomination. Hii mambo ya nomination, hii mambo ya nomination katika Kenya, new Kenya ambao tunaenda na hii Katiba ambao tunatengeneza saa hii, hii mambo ya nomination ikwishe kwa sababu mimi naweza ku-nominate rafiki yangu au relative fulani na kesho mimi namupandisha job kua Waziri, Waziri wanakula pesa mingi halafu kesho nalia pesa imekwisha serikali imefirisika, kumbe ni udanganyifu au ujanja ujanja, hiyo mambo ya nomination mtu achaguliwe tu na raia, kama anaanguka ameanguka. Mimi nafikiri yangu imekuisha, mimi naitwa Charles Mbwabi.

**Com. Maranga:** Asante mzee wangu weka sahihi hapo. Tunataka Shiembekho Shashita, majina marefu haya na ni magumu kweli, halafu atafwatiwa na William Shimenga ama huyu alizungumuza, William alizungumuza? Ni wewe? Okay utafuata.

**Shiembekho Shashita:** Mukenya wetu wa Katiba ni asante sana kukuja hapa, jina langu ni hiyo Shiembekho Shashita ninatoka sub location ....Kambini location. Ni asante Bwana Commissioner, ya kwanza uju mukoa huu ilikua imetupwa imesahuliwa hata sijui watu wa juu kama wanajua kuna watu kama hawa ambo wanaonekana uso kama yao. Shida ambyo iko kwa hii mukoa ni kitu kimoja, sisi watu ya Kenya sitini na tatu tulikua na mafafanuo uhuru imeingia na hii uhuru imeingia kando ya ....ya watu haikuingia kwa uso, tunaomba hapa Kenya wnapewa ...na kitambulisho na sisi watu wa ....tungetaka loan tunaambiwa kwanza leta title deed na hii watu ambo wanafanya hapa business kubwa biashara ni watu wa kitambulisho

wanachukulia pesa za Kenya. Mimi kama moja na sikitiza sana hata wako hapa Kambiri hawana shamba nchi hii hata point hawana lakini wanatumia pesa za Kenya kwa loan na mimi .....sasa nitauliza .....hapo Bwana Commissioner, tunasinyua kwa sababu sisi uhuru iko kwa bavu hapan iko kwa uso. Hiyo neno tuna .....sasa kwa masikio, kwa roho yetu kama mimi mmoja.

**Com. Maranga:** Unataka kuniambia hamuna title deed?

**Shiembekho Shashita:** Tuna title deed lakini nasikitika mimi nikiataka loan nitaulizwa title deed---

**Com. Maranga:** Na wengine hawaulizwie?

**Shiembekho Shashita:** Na wengine hawaulizwie wanapeana kitambulisho tu. Ya kufuata kwa hiyo maneno, wakati watu ya hapa Western Ileho division, kwa Shinyalu division ndiyo walikupatia hikupatia hi musiti wanaweka katikati tunamatatizo imeingia juzi juzi kuhusu hii watu ambaye wamazingira hii musitu kamba yake ni Shinyalu division na Ileho division. Hawa watu ngombe zao zilikua zinakunywa maji hapa.....hawa watu walikua wanatoa kuni kwa misitu, sasa Bwana Commissioner, hizi ngombe zikipatikana huko zinaenda maji zitabebwa zitaenda kulala sehemu ingine .....kama week moja ngombe zimefungiwa hiyo maneno inaumiza wale watu wanakaa round ya hii msitu. Na sijui hii mimi zinatengenezwa na nani, sijui ni ya mtu binadamu mwenyewe ama ni ya serikali na hii watu mwezi jana tunaomba serikali ya nchi hii elfu mbili zikapelekwa huko .....zidakufaa, hakuna hatua zimecukuliwa.

Nahizo ngombe hazikupelekwa courtini mtu alikua ana wekwa hapo na karatasi wewe mwaka zako ni ngapi na anlipa tu kwa huyo mtu kwenda chagua ngombe zako. Hii Bwana Commissioner, kama ni uhuru inataka iwe uhuru ya imani kwa binadamu. Sisi ambao watu ya Ileho division mwaka ingine tulikua hapa na Mungu moja hata nikiuza hii.....buru alinyima hapa miwa akapanda akaondoka na hiyo mali mpaka kwake na sisi watu wa nchi hii tukitaka hii shamba tupewe inakua ni kikwasa kwa watu wa Western.

Inginge Commissioner, kutoka hapa kama unajua hii watu tunakutuma uende kufungua hiyo mlango kama inafikiriwa .....kwenda kata iwe wazi kwa sababu yake unaona kama Elgon, mulima Elgon, nimetembea, watu ingine huko wanalima .....kwa hiyo msitu huko hakuna mazui ngombe zinakula huko, hii si msitu ya forest? Kuja hapa Kiangui watu wanalima hapa karibu na sisi kwa forest wana.....ndani na nini wanachota. Hii musitu kama hii ya Western hapo Bwana Commissioner tume shanga hata tumeshindwa sisi ni .....sisi hapana watu wa Kenya? Na hapa musitu yetu hii hakuna ndovu ndani, hakuna nyati ndani, hakuna chui ndani ni nugu zinatoka huko zinakuja kula mahindi yetu, bahati mbaya mtoto akiua hiyo nugu ni reserve itakuja kwako, .....nugu tangu imetoka huko musitu kama hapa inakuja chukua chakula yangu, tutafanya namna gani? Hapo tunashida kubwa sana Bwana Commissioner, tuna shida kabisa kabisa kuhusu hii upaka wakati iliingia hapa inanyayasa kila mtu hata yule anakaa kilometre sita kwa hiyo musitu ananyayaswa na hii watu wa bank.

Na nikimalizia, si kusema na makosa hakuna mtu ya Western anafanya kazi na hii watu hata sijui mtu akichagua hii watu wanatoka mbali na mimi najua Bwana Mwashimiwa Commissioner, hata sa ingine watona hii ngurue wataita ni boko na hawa hawajui ngurue na boko. Matatizo hii inatusumbua sana.

**Com. Maranga:** Asante Mzee wangu hayo tumeyasika.

**Shiembekho Shashita:** Ya pili nikimalizia kitu kidogo, ndugu yangu tumezaliwa na ndugu tumegawana shamba na mama na baba ....wewe utakaa hapa wewe na kaa hapa, tunaomba Bwana Commissioner, ukienda juu kurekibisha hii mambo hatutuaki ndugu yangu kuuza shamba bila kufahamisha wandugu zake sababu ya kuuza hiyo shamba. Anakula hiyo pesa huko Kisumu ama hapa town anarudi anakuja kusumbua mini patia mini mahali ya kuzika mwili yangu. Tunaomba hiyo maneno irekebishwe.

**Com. Maranga:** Asante Mzee wangu, maoni umetoa na yamefika kuja weka sahihi hapo. William Shimenga hata fuatiwa na na Gladys Mbaya, Gladys ako? Basi awe tayari.

**William Shimenga:** Bwana Commissioner, mimi kwa majina ni William Shimenga, Vice Chairman wa FORD KENYA katika Shinyalu. Mimi nitazungumuza kuhusu the three arms of the Government, Executive, Parliament and Judiciary. Hizi three arms hatuwezi kusema ziko independent because utakuta Executive is the product of Parliament and the Judiciary is an appointee of the Executive. In this case haziwezi kua independent.

**Com. Maranga:** So, what are you suggesting?

**William Shimenga:** Na suggest tunazagana ziwe completely independent mtu awe wa parliament awe tu Mbunge, Executive hazi-appoint mtu kwa Judiciary ama awe nominated. Section 25 and 6 and 51 of the Katiba inatakikana irekebishwe.

Elected members of Parliament ni watu wa raia si watu wa President, kwa hivyo President hawezi kuvunja Bunge bila raia kujua inatakikana Bunge iwe continuous kwa mtu fulani ijilikane Bunge itazungumuza kutoka hapa mpaka kufika hapa iwe na-terms mtu zake kama vile shule ziko na terms, first term, second term, kitu kama hiyo, vunja isi vunjwe vujwe tu bure na President. Nominated MP's; Hawa nominated MP's haitakikani wawe wapewe kiti kama ya ministerial post because they are only nominated by.....an individual na wakipewa kazi ya serikali hawawezi kutumia raia kwa maana alikua nominated na atatumia yule mtu ambaye alimu-nominate hapo kwa hivyo nataka huyo asipewe kazi ya serikali.

Nitaongea kuhusu election period. Election period inatakikana ijulikane isiwe tool ya mtu natakikana kama wakati huu tuwe tayari tunajua election ni tarehe gapi mwezi gani, isiwe tool kwa mtu individual.

**Com. Maranga:** Unatarehe yoyote ambayo unataka kupendekeza?

**William Shimenga:** Naweza kupendekeza tu wakati wa December wakati wa holiday bora tu shule zimefungwa.

**Com. Maranga:** Lakini December unajua watu wanenda Christmas, kama Waluyha wankuja wote wanawacha Nairobi wazi.

**William Simenga:** Baada ya Christmas. Baada ya Christmas you Lordship. Haya Pblc Commission; Public Commission hiyo ni Commission ya public, sasa ikiwa ni public itakuwache tusijue ni report gani ilipata hiyo report inaenda kwa mtu anaweka huko na ilikua public, nini maana ya public? Hiyo inatakikana itangazwe tujue ni kitu gani hiyo Commission ilichunguza na ilifika wapi na ilikua namna gani.

Pengine na weza kukilia tu mukazo kwa hii mambo ya pombe ya kienyeji. Hii pombe ya kienyeji na taka, ningependekeza iruhusiwe kwa maana tunafunga ama iko banned na lakini si kwamba haiko, iko imetengenezwa---

**Com. Maranga:** Lakini wewe unaonekana mzee wa kanisa.

**William Shimenga:** Ndiyo mimi ni mzee wa kanisa lakini ninazungumuza kwa wale wenye hawatumi, wako wanatumia.

**Com. Maranga:** Si wewe munatakikia muleta hawa watu kwa kanisa wawache kukula hiyo kitu? Okay endelea.

**William Shimenga:** Hii pombe ya kienyeji Bwana Commissioner, inatakikana tu iruhusiwe kwa maana tunasema tume-ban lakini inatengenezwa na mtu fulani ama askari anaenda kushika yule mtu na analipa kitu kidogo kwa hiyo mtu afadhali iruhusiwe na ushuru iwe isiende kwa serikali.

**Com. Maranga:** Haya asante, ya mwisho.

**William Shimenga:** Ya mwisho----

**Com. Maranga: (interjection)** Unjua nyinyi ni wanasiasa hamuezi mukamaliza. Ya mwisho.

**William Shimenga:** Ya mwisho Mweshimiwa, hii ni Attorney General. Attorney General kama legal advisor to the state hatuwezi kumupa nguvu sana a-discontinue casi wakati date inaendelea, kama casi imeamulishwa iendele iende na imalizke na kama ame discontinue ile ya serikali mimi binafsi nikipeleka case yangu courtini nime tumia pesa yangu asikatishe mimi kwa maana kama yeye akikata kuendesha hiyo casi then kulikua na kitu fulani alificha na mimi nikitaka kusumbua hiyo kitu aniwache.

Thank you you Lordship.



**Com. Maranga:** Asante weka sahihi na utupee hiyo meorandum. Gladys Mbaya.

**Gladys Mbaya:** Kwa majini mimi ni Gladys Mbaya nikiwa .....location. Niko tu na point karibu tatu hivi venye nilifikiria nikipeane kwenyu Sir, ya kwanza ni kitu kuhusu compensation kwa mfano kwa forest. Kuna nyama zinakula vyakula zetu hata zingine zinakula watoto wetu hata na watu wetu na wanenda tu bure hakuna malipo. Tungependa destruction yenye inafanyiwa .....forest serikali yetu ipeane compensation pia nikiwa kwa forest especially game reserves, kuna ushuri yenye inatolewa kwa milango ukitaka kuingia tuseme kama hapa Buyale anapeanako kitu kidogo ndiyo uingie uende uone vitu venye viko kwa forest, ningependa hizo pesa zirudi kwa communities within the forest ili waendeleze na maendelo yao kwa maana wamenyimwa nafasi ya kuingia kwa forest kwa hivyo zile pesa kidogo yenye inatolewa tungependa ipatiwe the communities within the forest ili nao waendeleze muradi yao.

Lingine, pia kwa hii forest ningependa wakati wanafanya recruitment wawe wakichukua zile communities zenye zinakaa kwa forest kwa mara tuko na watoto wamesoma na wakati wana-recruit hawa askari wa forest utakuta mtu ametoka mbali huko anakuja ana kua askari kwa forest sasa unashindwa na hawa wenye wanasoma wenye hawawzi waka kua askari wa kulinda hii msitu?

Na mwisho kwa upande wa mama kama saa hii vile inflation iko sana tunependelea ikiwzekana wamama wasetiwe banking system yao kando, yaani yenye iko na low rates ili wamama wajisikie ya kwamba hata wakienda kufungua, wakifungua za bank yenye itatoshea kwa maana saa hii ukienda kwa bank wanakuambia ukitaka kufungua account ufungwe na pesa hii hata zenye huna kwa hivyo ningependa kwa upande wa akina mama tu setiwe banking system yetu iwe kwa mapato yetu kulingana na sis wakina mama.

Na hii nayo sikuandika isipokua imekuja tu ningependa hizi viti ya wakati wanakua nominated heri zipatiwe sana sana wakina mama kwa maana wakati tunafanye campaign ili wamama waendeko Bunge au wawe coucillors tunashidwa sana na wazee kwa hivyo heri tupatiwe special seats kwa upande wa councillor shift na Ubunge ili wamama nao yaani hata akishindwa lakini mama asetive nafasi yake kwa Bunge au kwa u-councillor. Ni hayo tu asante.

**Com. Maranga:** Asante mama karibu na uweke sahihi na utupe hiyo memorandum. Richard Isiahu halafu atafuatiwa na Pascal Lusuli. Pascal ako? Okay utafuata.

**Richard Akwenda:** Bwana Commissioner, na wengine wote walioko nina machache karibu mawli hivi nitasema na kwa majina mimi naitwa Richard Akwenda Isiahu. Mimi nitazugumuza kwa upande ya matajiri wetu hapa Kenya na wale ambayo wanyjiyakulia mashamba kubwa kubwa. Langu la kwanza ni hivi, hasa kwa hawa matajiri ambaye wako hapa Kenya hata hawa wa Kihindi, Waafrika wetu ndiyo sasa wamechangia sana kwa umaskini wa Kenya. Wamefinya sisi wafanyikazi,

tunapata mshahara kidogo na kazi ni nyingi pia ukienda kwa upande mwingine utapata hao matajiri alikufukuza kazi na umefanyia karibu miaka ishirini utakuja kupata hawa wandugu zetu labour na NSSF pia hawa wamechangia kwa hawa matajiri wana jiunga wanakua kitu kimoja pengine wamemufuta nyinyi wafanyikazi mia mbili hivi na mutajikuta ya kwamba sasa hamuko mahali.

Offisi ya labour na offisi ya NSSF wamejiweka pamoja mtatoka bila kitu sasa mtu wa labour ndiyo atapata kitu, mtu wa NSSF ndiyo atapata kitu, kwa hivyo ningependa hizo offisi mbili na hizo pesa zingine mujaribu kupika mzaza manake wamechangia sana kueneza njia ambaye munasema ile muchango ya kisadi. Mukirudi upande wa watoto, pia ya faa mzazi kama umewachishwa kazi upewe haki yako hata kama ingalao ni kitu kidogo ili pia huyu mtoto aendele na masomo yake. Bila hiyo watoto hawawezi kusoma vile munasema mutataka watoto wakule vizuri wasome vizuri, watakulaje na mimi mumenipiga teke nje huyu tajari anakuambia hata enda kwa offisi ya President ama kwa Ministry of Labour na kweli ukienda kwa huko uwezi pata kitu.

Ningefanya marekebisha hapo matajiri pia wapate sheria katika ...nakutuwekea na kuchangia muchango ya kuweka NSSF na ingineo yote hii uchumi yetu intapanda juu kuliko mtu moja kula hiyo. Na nikirudi mahali pengine, nita rudi kwa upande ya barabara zetu za Kenya kwamba munasema zimekua nini ni nini accident mingi ma-driver nini la, hapo ningependa mukirudi huko mwambie ya kwamba barabara zetu za Kenya zimechangia kua bofu ndiyo vile tunapata accident nyinigi tena pia ma-driver wetu na wafanyikazi wengine, unapewa mda fulani uondke hapo ufike Kampala baada ya siku moja na unapata barabara yetu ya Kenya inamashimo mengi kwa hivyo unasikia accident imetokea hiyo pia muchangie kuaangalia masilahi ya wafanyi kazi ambayo sisi tunafanye kazi ndefu mimi nikiwa mmoja wao, nimewai kutembelea karibu Africa zima ukiangalia hapa Kenya tuko na mabarabara bofu sana lakini ukingia hapa majimi zetu wako na barabara safi. Pia muangalie hiyo.

Nikienda mahali pengine---

**Com. Maranga: (interjection)** Na ya mwisho.

**Richard Akwenda:** Ni ya mwisho pia. Tuko na matajiri hapa wamejinyakulia mashamba acre arubaini, acre ishirini lakini ukianza kufika tarubini utakuta umaskini ime kua mengi, huu tajiri amenyakua shamba ametupa wale watu walikua kwa hiyo shamba wamekaa kwa barabara kwa mufano, pita kwa Athi River, kuna ma-squatter kwa barabara, pita kwa barabara mzee alienda juzi kuanzi Soie kuna ma-squatter wamtupwo barabarani kuja hapa.....utakuta ma-squatter wametupwo barabarani.

**Com. Maranga:** Unapendekeza nini?

**Richard Akwenda:** Mimi ningependekeza kwa hayo mashamba, mimi nina acre elfu mia moja ama acre elfu ishirini, ni heri mungeenda mujadiliane na hawa watu pia hizo mashamba wagawiana hawa watu ma-squatter ama mutujenge ingalao factory

kama hii sehemu yetu hatuna hapa factory moja tuko na miwa, tuko na chai, tuko na kahawa lakini factory ikija umesikia umerushwa imenda wapi? Inenda kwa Waturkana.

**Com. Maranga:** Lakini mzee mimi nakuliza, sasa wewe tukipatia squatters wote shamba yaani hiyo itamanisha kweli squatters wataisha Kenya hii na wengine wale ambao baada yawe squatters kumalizika?

**Richard Akwenda:** Asante sana hapo uesema vizuri.

**Com. Maranga:** Tutafanyje?

**Richard Akwanda:** Kitu tungefanya, Kenya yetu hii ninamashamba makubwa sana kwa mufano mimi niko na acre elfu mia moja kwa nini sigawie ma-squatter? Alikuta msichana moja? Nakujibu.

**Com. Maranga:** Sawa, huyu wa elfu mia moja aki.....hiyo, apeame na tukishamliza kupena kabisa sasa ingine itatoka wapi kwa sababu watu wanazidi kuzaa

**Richard Akwanda:** Bado si kwa nyingi, yule atapata mubaya atamupatia huu squatter mahali ambapo hii ametoka vile sisi wazee wmetuwachie hapa.

**Com. Maranga:** Okay, asante basi weka sahihi vitabu vyetu. Tupate Pacle Lusuli halafu afwatiwe na Joseph Ikomeli. Joseph ako? Okay, uwe karibu, haya haraka haraka toa maoni yako.

**Pascal Lusuli:** Commissioner, na wananchi wenzangu, hamujambo? Mimi nina maoni kama matatu hivi---

**Com. Maranga:** Jina?

**Pascal Lusuli:** Jina ni Pascal Lusuli.

**Com. Maranga:** Haya toa maoni yako.

**Pascal Lusuli:** Kutoka Lukusi sub location. Maoni yangu ya kwanza ni kwamba kuhusu Katiba kwa sababu nasema tubadilsho Katiba na ukiangalia sana sana hapa vile tumekaa tuko kwa Katiba na wengine wamesema iwe kama fuzo kwa schools na hawazungumuzi kuhusu wazee kwa sababu hapa hakuna wazee ambao wanawza kukuja kwa juu ya juu ya Katiba na wako wanabaki nyumbani lakini kwa kua hawajui maana ya Katiba wamebaki nyumbani kwa sababu watukuja na kitu hawajui. Mimi kupendekeza kwangu ningiona Katiba wnagechapisha vitu kama vitabu vidogo halafu ziwe distributed kwa

ma-Chief au ma-Assistant Chief ili wakiita mukutano au baraza wafundishe hawa wazee kwa sababu wazee ndiyo wanakuja wengi katika barazaa ya ma-Chief wawafundishe kuhusu Katiba kwa sababu ukiagalia hapa na wazee na tumekuja kuhusu Katiba.

Jambo la pili, tunasema kweli tuko uhuru na tumepata uhuru lakini ukiangalia sana sana kama sisi wananchi wa kawaida ni kama ambaye hatujapata uhuru kwa sababu ya kusema hivyo unakuta mzee au mtu fulani yuko na shamba lake au yuko na boma lake nyumbani kwake halafu unakuta yuko na miti, amepnada miti yake na yuko na njaa anataka kukata hii miti kawaida achome makaa au apasuwe mbao unakutaa amechoma makaa ama amepasua mbao anataka kupeleka kule ambapo apate kitu kidogo cha kutumia unakuta huko njiani anasumbuliwa sana unakuta either Administration Police au Police sasa unashindwa mtu kama huyu na hii ametoa katika shamba lake hakuenda katika forest sasa unashindua ni kwa sababu anaishi karibu na forest au ni sababu ni mtu ambaye hana kitu ama ni sabu gani anasumbuliwa na jambo kama hilo kwa sababu ni kitu anabarua na amebeba makaa na anapeleka kwenda kuuza lakini unakuta anasumbuliwa na ni jasho lake na ametoka kwa shamba lake sasa unakuta na Chief yuko na ndiyo alimupa hiyo barua yuko na barua ya Chief, yuko na barua ya sub-Chief, yuko na barua ati ya DO lakini unakuta anayanyshwa huko njiani sasa unashindua tuko uhuru kweli?

Jambo la tatu, ningezungumuza kuhusu hawa watoto munasema chokora jinsi wanvopatikana kwa sababu ukitembea katika mijini watoto chokora wako wengi sana.

**Com. Maranga:** Tunjua wanapatikana kwan jia gani lakini tunataka utoe mapendekezo, unataka tuwafanyie nini?

**Pascal Lsuli:** Mapendekezo yangu vile wangefanyiwa au jinisi tungejaribu kusuluhisha chokora wasiwekwo unakuta mzazi kwa sababu hawa ndiyo wenye hao watoto sasa huyu mtoto anapatikanaji kua town mpaka anakua chokora? Tuangalie tue na sheria fulani kuangalia mzazi kama ameza watoto tuwajibu wake apeleke huyu mtoto kuenda shuleni kwa sababu akienda shule hata kua na wakati wa kuenda kuzunguka zunguka mpaka awe chokora. Hayo ndiyo maoni yangu ningependekeza.

**Com. Maranga:** Asante nashukuru weka sahihi na utupatie memorandum. Joseph Ikomeli karibu halafu utafutiwa na Fabian.

**Joseph Ikomeli:** .....hamujamboni wote?

**Com. Maranga:** Fabian Chite? Iko? Karibu.

**Joseph Ikomeli:** .....ni nayo----

**Com. Maranga: (interjection)** Anza kwa majina mzee.

**Joseph Ikomeli:** Mimi ni Joseph Koniri Lukhalo na naishi.....mimi hapa ninayo ...mbele yenyu mimi nakaa hapa nikanunua shamba huko mbali niko mbali na forest alafu taabu nilikua nayo niko.....na niko na mtoto kwa ndani ya school.

**Com. Maranga:** Ongea kwa mke kwa sababu tuna record.

**Joseph Ikomeli:** Nina mtoto kwa school halafu hii mtoto ndani ya school iko secondary na mimi nilikufia mama yako na kweli nilifanya bidi nikapanda shamba yangu ni shamba kubua.....nikapanda miti na iko miti ingine ile ya kienyeji ya kizamani ningefikiria nitafanya nini na mimi ni mzee vile unaniona hivi sasa mimi niko na mwaka sabini na sita mimi nimezaliwa nilizaliwa ishirini na tano ukifanya ishabu. Basi, nilitoka moja kwa moja nikaenda kwa Likuru, nikamwambia Likuru hii miti yangu nataka nifanye kazi.....Likuru akasema ningona kweli kwenda ona Sub Chief, nikaona Sub Chief , Sub Chief ako.....nikaenda kwa Chief, Chief alikubali, nikaenda kwa DO, DO akakubali yes. Wakati niliona kujua kukata hiyo miti hakuna.....manake nitalimo hiyo juzi juzi hiyo nikakmatwa na hiyo makaa ngunia ishirini wanataka ni-draw fine shillingi elfu ine, hiyo makaa ilicukuliwa ikaenda na ile watoto walika wana.....makaa hiyo wakafungwa ndani mwezi mbili. Sasa hiyo .....ndiyo unaona katika Kenya yetu tutafanya nini hiyo ni yangu ya nyumbani sisi na kaa karibu kwa forest na hawa watawala wote wamesha pata wamesha pewa mimi report sema kuenda fano wakati .....sasa mimi na shikua tena baada ya Sub Chief akipea mimi nafasi Chief amshapea mimi nafasi Chief amshapea mimi nafasi tuende hapo watu wa KEPI wanachika wewe.

**Com. Maranga:** Hiyo watu walichgka wewe ni watu wa forest ama game---

**Joseph Ikomeli:** Hapana. Askari ya KEPI, ya .....na watu ya KEM.

**Com. Maranga:** Kwa hivyo watu wa Administration Police?

**Joseph Ikomeli:** Basi, wanasema pia---

**Com. Maranga: (interjection)** Ulirudi kwa DO?

**Joseph Ikomeli:** Kurudi kwa DO pia wanaseme.....

**Com. Maranga:** Ni huyu huyu, yuko wapi?

**Joseph Ikomeli:** Sasa yeye amepata transfer, halafu Chief sasa kutoa barua ingine Chief akakopa kwa maana sasa inaonekana saaa inngine anaweza kuharibu kazi yake ndiyo mimi naona nifike hapa kwenyu then katika ndani ya Kenya mali yako imebaki hapa ndiyo unapata...utapeleka wapi sasa.

**Com. Maranga:** Na hiyo case ilikua Kakamega? Case ulichukulia wapi? Kakamega? Ulichukuliwa courtini wapi?

**Joseph Ikomeli:** Hiyo unapeleka kwa camp yao haiendi Kakamega.

**Com. Maranga:** Kwa hivyo hiyo ni Kangaroo Court, ulipigiwa fine wapi?

**Joseph Ikomeli:** Fine walipiga sisi hapo hapo wanapiganga fine kwao hapo kwa camp yao.

**Com. Maranga:** Haya, wewe utaongea na hiyo DO hapo inje halafu---

**Joseph Ikomeli:** Sasa hapo nikisema hiyo hawataki kusikia maana wanasema sio hi siko kazi yetu sasa uende kwa officer ya forest anashika wewe ukikuja upande wa Polisi, Polisi inashika wewe, ukikuja upande ya KEM, KEM inashika wewe, ukienda upande wa.....inashika wewe, sasa utafanyje hapo katikati na mahali wewe, niko nyumbani sasa niko ma miaka karibu kumi na tano kwa sababu mama amekufa na mimi nimebakia na watoto hao mimi mwenyewe na lisha sasa mimi na kwisha nguvu ya kufanya kazi mimi nilikua kazi ya driver ya kuenda huko Zaire, kurudi hapa sasa nguvu yangu imekwisha.

**Com. Maranga:** Lakini una miti yako kwa shamba yako?

**Joseph Ikomeli:** Sasa natmia shamba yangu.

**Com. Maranga:** Sasa kuna DO mupya utamuona halafu kwa sababu hata Minister alikubali ukipewa kibali unakata miti yako bora tu usikate mingi uharibu, unakata halafu unatumia kwa matumizi yako bora tu hapana haribu ile environment lakini uwe umeona District Environmental Officer, si ni hivi Bwana DO?

**DO:** Yes, kama ni yake, ni yake tunakua tunaomba permit.

**Com. Maranga:** Hiyo permit yeye anasema alipewa halafu Chief naye akamupa hata Assistant Chief hata kwa DO lakini alishikua baadaye, alichoma makaa wakachukua makaa----

**DO:** (interjection inaudible)

**Com. Maranga:** Sasa wakati huu hakuna tabu sasa.

**Joseph Ikomeli:** Kwa hapo ile barua walichukua wakararua.

**Com. Maranga:** Sawa, sasa tutona DO mpya. Kuna DO mwingine anaelewa hiyo maneno na inaonekana yeye anaelimika vizuri ata kusaidia.

**Joseph Ikomeli:** Sasa ndiyo mimi naomba hapa kazi ili minigine ndiyo mimi nishanguza hata makaa ingine ninayo nymbani huko na kaa, nitafanyaje?

**Com. Maranga:** Enda offisi kesho. Okay? Asante weka shahihi. Fabian Chite halafu atafuatiwa na Jacob Lukano, Jacob ako? Kama hayuko huyu niamusahao. Fabian Chite, haya toa maoni yako kwa ufupi na kwa ukweli.

**Fabian Chite:** Asante sana Bwana Commissioner, Bwana DO na wenzangu muko hapa.

**Com. Maranga:** Majina yako kamili.

**Fabian Chite:** Jina yangu ni Fabian Chite mimi mukaji wa hapa. Nina maoni matatu lakini nilikua nayo nyingi nimesikia wenzangu wanasema. Nashukuru kwanza ningepomba Commissioner kwa maoni tunazaa vijana na vijana wengi wako idle hawana kazi na nafikiria tu-organize hili national services tu-recruit hawa vijana waende kwa national services wafundishwe kazi ile itawasaidia instead kukaa kwa barabara kukua idle baadaye watukua watoto wabaya.

Inginge sema lakini wame sema ingawa nitarudia ningependa terms ya MP na councillors ningefikiria wananchi...mkono kuwapeleka kwa Bunge au kwa council wanabunge anafanya kazi hata si sawa amenda huko shauri ya mshahara. Ningefikiria Commissioner, tuwe na power tumuitie huyu Bwana tuchague mwingine within less than two years kama mwenzangu amezungumuza hapa mbeleni tujaribu mwingine kabla haja reach miaka mitano huko ningependelea hivi hivyo councillor kama hafai asikae huko mpaka miaka mitano na anatumaribia area yetu.

Ya mwisho, tuombe Commissioner, wengine wamesema mambo ya majimbo. Ningependelea maoni yangu tungekua na serikali si ya majimbo kwa sababu tukifanya majimbo italetu chuki, italetu watu bila kuelewana na hii miaka tumekaa kwa uhuru ni mingi. Ningependelea wengine wamesema tue na Prime Minister, naona hiyo ni bure afadhali tuendele tue na President elected na tue na Vice President elected. Hawa wata fanya kazi na itatusaidia. Kwa hayo machache nimeshukuru, asante.

**Com. Maranga:** Asante, weka sahihi na utupatie memorandum. Jacob Lukano, wewe ukienda kutembea tutapita wewe na hatutaita wewe tena.

**Jacob Lukano:** Kwa majina ni Jacob Lukano. Maoni yangu, serikali imekua sana. Moja, mimi ni mukulima napanda mboga, ikipelekwa sokoni mboga ya shillingi hamsini serikali inachukua ushuru shillingi ishirini na baki na thalathini.

Kwa local government ndiyo inamaliza sisi kabisa.

**Com. Maranga:** Wanatakajee, unataka itupiliwe mbali?

**Jacob Lukano:** Local government ufanye tu kama vitu imetandikwa sokoni wafanye tu ushuru mwaka moja si ati nimepeleka mboga ya shilingi ishirini na local government inachukua shilingi ishirini sasa natoka hapa with totally nothing nitabaki bure. Hiyo ya kwanza.

Ya pili, maoni yangu naona kienda courtini ukae huko maasa ishirini na nne maasa hii ishirini na tano upelekwe cortini, courti imaliza uamuzi sio ati ukae from Monday masiku kumi na nne halafu mwisho yake ionekane ya kwamba wewe hakuna makosa.

Tatu, Police wasikimbishe watu na bunduki kwa makosa ndogo ndogo, kuna makosa kama kuiba, kuua mtu wakimbishe mtu na bunduki na kubora maji lakini makosa ya kinyumbani askari asionekane na bunduki kwa maboma ya watu akirandaranda hovy hovy.

Nne, mabarabara, mabarabara serikali itende tu pesa na igawanye kwa ma-province wakati wa budget. Wakigawanya budget watende tu Western Province pesa ya barabara kiasi fulani, North Eastern kiasi fulani, hiyo ionekane hadarani pesa inakuja kutengeneza mabarabara ma-million fulani Western Province ama Nyanza namna hiyo.

Na ya mwisho, President asichague Vice President. Vice President kwa mufano, President akitoka Coast Vice atoke Rift Valley, President akitoka Rift Valley Vice atoke Nyanza. Yangu ni hiyo.

**Com. Maranga:** Thank you, kuja hapa uweka sahihi Lukano. Sasa anayefuata ni Julius Lihanda. Karibu utafwatiwa na Bernard, nani huyo sijui ni Muyeno, Muyeno ako? Okay you will be next and your names are tough.

**Julius Lihanda:** Bwana Commissioner, majina yangu ni Julius Lihanda natoka sehemu za.....kambiri location. I do not have a written memorandum niko na mambo mawili matatu yale ambyo nitaguzia.

Jambo la kwanza ni kwamba tunazungumuzia mambo ya Katiba ambyo wengine ambayo tuko katika area hii yao tumekua hapa tukitoa maoni. Ukweli ni kwamba hatujui hiyo Katiba inazungumzia nini. Ingelikua au ingelifa vile mwenzangu hawa wawili wamezungumzia tue na Katiba ambyo kila mwanchi wa Kenya tuijue inaguzia nini inazungumzia nini katika idhara zote ambazo zinahusika na serikali ili.....tunapotoa maoni au tunataka kubadilisha sehemu fulani unajua sehemu fulani inasema hivi na tunataka iwe hivi, kwa hivyo we are talking of the Review of the Constitution ambaye hatujui kwa hivyo hata kama tutapendekeza Katiba ingine iundwe mpya tungelihitaji yale ambaye tunaguzia kila mwananchi wa Kenya aweze kujua Katiba



hiyo inazungumuzia nini.

Na mambo ya Parliament kuweza ku-amend tungelihitaji referendums wale ambaye tutaguzia haya mambo ya Katiba tupewe hiyo nafasi ya kufanya amendments katika Katiba yetu. Jambo lingine ni mambo ya ufisaidi huu ambayo tumelia viliyo vimkuepo ni ajabu sana mtu kuiba pesa za uma ma milioni ya pesa na unasikia kwamba sheria inasema unakuta huyu mtu hiyo pesa ameziweka katika account number ya mukewe au za watoto. Mtoto wa miaka sita anaweza kua na million sita kwa account? Unashindwa huyo mtoto kwani yeye anafanya kazi wapi kwa hivyo unakuta ya kwamba sheria inasema yeye hawezi kustakiwa mama au mwanamke wa huyu bwana aliiba pesa hawezi kustakiwa. Tungelihitaji sheria iwekwe ya kwamba hata kama huyu ni mama aliowekewa hiyo account astakiwe maana hiyo pesa sio zake.

Jambo lingine nilitaka niguzie kidogo ni mambo ya sheria ambaye imepitizwa na hiyo inaumiza sisi sana wanaume ya kwamba ukumulazimisha mukeo katika hali ya ngona bila yeye yani kukubali unastakiwa ana uhuru ya kuenda kukustaki. There are some other men who ambao...katika shida kama hii wengine hata wanapigwa na wanawake na sheria haiguzie hiyo kwa hivyo tungelipenda ikiwa sheria imewekwa ya kwamba mwanaume ambaye anaweza kumulazimisha mukewe kua na ngono astakiwe hata nao pia wanawake wale ambaye wanalazimu wanaume au mabwana zao kua na hali hiyo pia nao wastakiwe. Kwa hivyo sheria isileme upande mmoja.

Jambo lingine tumeguzia mambo ya musitu na wengi wameguzia jambo hilo sitaki kulirudia sana lakini tungelipenda tue na uhuru wale ambao tunakaa karibu na musitu tuweze kupewa nafasi hiyo nzuri ya kuifadhi huo musitu ili rasimali ambazo zinatoka ndani wale ambao tunakaa karibu tuweze nasi kupata share yetu. Ni hayo machache ambaye ninazo.

**Com. Maranga:** Asante. Bernard.

**Bernard Muyeno:** Commissioner wetu na wageni wengine wote pamoja wazee, wamama habari zenu/

**Com. Maranga:** Anza kwa majina yako na uonge kwa mike naona wewe ni mrefu.

